# Nipashe

Jumatano Januari 30, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579828

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



## Taharuki mabomu yavunja mkutano wa naibu waziri

UKURASA 2




UKURASA 13

# DC kumweka mtu ndani kwa saa 24 si haki-JPM



UKURASA 2



Majaji wapya wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu wakiapa kiapo cha uadilifu kwa viongozi wa umma mbele ya Rais John Magufuli baada ya kuwaapisha Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mashtaka mapya 100 vigogo wa Nida

UKURASA 2

## Mambo 4 muswada Sheria ya Vyama

UKURASA 3

**MICHEZO** **MWINYI ZAHERA AITISHA SIMBA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM: Si haki DC kumweka mtu ndani bila kumfikisha kortini

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli, maarufu JPM, amewataka wakuu wa wilaya kutumia vizuri madaraka yao, akieleza kuwa si haki mtu kuwekwa ndani kwa saa 24 kisha kuachiwa pasipo kufikishwa mahakamani.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam katika hafla ya kuwaapisha majaji na viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni, wakiwamo wakuu wa wilaya wawili, wakurugenzi 10, majaji wa Mahakama ya Rufani sita na majaji wa Mahakama Kuu 15.

Rais Magufuli aliwataka wakuu wa wilaya aliowateua hivi karibuni, kwenda kusimamia sheria na kutotumia vibaya madaraka kuweka watu ndani ya mahabusu ya polisi.

Alisema kitendo cha mkuu wa wilaya kumweka mtu mahabusu kisha kumtoa bila ya kumshitaki mahakamani si haki.

"Wakuu wa wilaya mna sheria na mamlaka mlizopewa. Msizitumie vibaya, sheria za kuweka watu ndani mnazo, lakini msizitumie vibaya. Mtu anawekwa ndani, halafu baadaye unamtoa, eti ameshajifunza, hujampeleka mahakamani, 'it is not fair' (si haki)," Rais Magufuli alisema.

Aliongeza: "Viongozi wengi wamezungumza kuhusu hili, na mimi narudia, kama una mamlaka ya kuweka watu ndani sawa, Je, mkuu wako wa mkoa na yeye akiamua kuweka ndani, si itakuwa ni vurugu? Kuna masuala mengine hayahitaji kuwekana ndani, yanahitaji maelekezo, hapa pawe hivi na pale pawe hivi."

Rais Magufuli pia aliwataka wakurugenzi wapya kwenda kusimamia ukusanyaji wa mapato na kutojihusisha na malumbano na wakuu wa wilaya.

'Tumefanya mabadiliko madogo kwenye wilaya mbili, wilaya ya Mwanga kila mtu amesikia, kuna wakati DAS aliwekwa ndani, mara mkurugenzi, vurugu zote ukizifuatilia zinaanza na mkuu wa wilaya," alisema.

Aliongeza: "Lakini, yeye ni mtaalamu wa wadudu, amesomea wadudu, nikasema labda huwa anawaona watu wote ni wadudu.

"Nikaamua kumpeleka sekta ya wadudu, labda atafanya vizuri, na hata kwenye mazungumzo yake anasema yeye ni mtaalamu pekee wa wadudu Tanzania."

**SABABU KUPEWA UJAJI**

Rais Magufuli pia alieleza sababu ya kuwateua kuwa majaji mahakimu mawili; Upendo Elly na Athumani Kirati. Alisema kuwa, katika utumishi wao wa uhakimu, wawili hao walizingatia maadili ya kazi na kufanya kazi kwa kujituma.

Alisema Jaji Upendo, wakati akiwa hakimu mkoani Shinyanga, alisimama imara katika kesi ya uchakachuaji su-

INAENDELEA UK.8



Askari polisi kitengo cha usalama barabarani, akiangalia taa za kuongezea magari baada ya kugongwa na gari la mwendokasi katika eneo la Magomeni Mapipa jijini Dar es Salaam jana, hakuna aliyejeruhiwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,

28 Januari, 2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatatu** tarehe **04/02/2019** kampuni ya **Mainline carriers Limited** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es Salaam Port** kuelekea **Tunduma**, gari hilo lenye namba za usajili:

   **T653DFA/T245BYM**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   Urefu - mita 20.0
   Upana - mita 4.3
   Kimo - mita 4.6

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaama Port hadi Tunduma Kupitia Mikumi,** gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

# Taharuki mabomu yavunja mkutano wa naibu waziri

**Na Romana Mallya**

TAHARUKI imeibuka baada ya mabomu ya machozi kupigwa jirani na mkutano wa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, mkoani Njombe.

Masauni aliitisha mkutano huo kwa lengo la kuzungumza na wananchi wa vijiji kulikotokea mauaji ya watoto 10 mkoani humo.

Wakati mkutano huo ukiendelea kwenye Viwanja vya Turbo mjini Njombe, ghafla jirani na mkutano huo kulisikika milio ya mabomu ya machozi, kitendo ambacho kilisababisha shughuli kusimama.

Baadhi ya wananchi waliokuwa kwenye mkutano huo, walisogea eneo ambako mabomu hayo yanapigwa kujua chanzo chake na baadaye kudai mbele ya naibu waziri huyo kuwa, kuna mama amekamatwa na mtoto ambaye si wake,

INAENDELEA UK.8

# Vigogo Nida wafunguliwa mashtaka mapya

**Hellen Mwango**

VIGOGO sita wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) akiwamo Mkurugenzi Mkuu wa zamani, Dickson Maimu, wamefikishwa mahakamani na kusomewa hati mpya ya mashtaka 100 yakiwamo 22 ya kughushi, nyaraka za kumdanganya mwajiri 43, kujipatia fedha mawili, matumizi mabaya moja na kutakatisha fedha na kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya Sh. bilioni 1.175.

Mbali na Maimu, washtakiwa wengine ni Aveline Mombuli, Astery Ndege, George Ntaliwa, Xavery Silverius maarufu kama Sliverius Kayombo na Sabina Nyoni.

Walisomewa mashtaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali, Simon Wankyo na Leonard Swai. Wankyo alidai kuwa kesi hiyo namba 07/2019 ina mashtaka 100 dhidi ya washtakiwa hao.

Alidai mshtakiwa wa kwanza, wa tatu, wanne na watano wanakabiliwa na mashtaka mawili ya kula njama la kwanza na la 85.

Alidai kuwa Maimu, Ndege na Ntalima wanakabiliwa na mashtaka 22 ya kughushi nyaraka malipo kutoka Nida.

Upande huo wa Jamhuri ulidai Maimu, Ndege na Ntalima wanakabiliwa na mashtaka 43 ya kuandaa nyaraka za uongo za malipo ya kumdanganya mwajiri wao.

Swai naye alidai Maimu, Ndege, Ntalima na Kayombo, wanakabiliwa na mashtaka 25 ya kutakatisha fedha haramu.

Aliendelea kudai katika mashtaka matano mshtakiwa Maimu, Ndege, Ntalima, Kayombo, Mombuli na Nyoni kwa nyakati tofauti waliisababishia Nida hasara ya Sh. 1,175,785,600 walishindwa kutimiza majukumu yao na kupitia nyadhifa walizokuwa nazo waliisababishia hasara hiyo.

Katika shtaka la 95, ilidaiwa kuwa kati ya Novemba 7, 2011, makao makuu ya Nida ofisi zilizopo Kinondoni, Maimu akiwa mtumishi wa umma kama Mkurugenzi Mkuu na Nyoni akiwa kama Mkurugenzi wa Sheria walitumia madaraka yao vibaya na kusababisha Shule ya Sheria na Kampuni ya M-S Law Partner kujipatia faida ya Sh. 899,935,494.

Ilidaiwa Juni 5, 2013 katika Benki ya CRDB tawi la Lumumba, Ilala jijini Dar es Salaam Kayombo kuwa alijipatia kwa njia ya udanganyifu Sh. 45,515,961, huku akijua ni mazalia ya kughushi na utakatishaji fedha haramu.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Swai alidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na aliomba mahakama kupanga tarehe ya kuwasomewa washtakiwa maelezo ya mashahidi.

Pia, alidai wameshawasilisha taarifa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa kuhusu kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu alisema washtakiwa watasomewa maelezo ya mashahidi Februari 12, mwaka huu na wapelekwe mahabusu.

Alisema mshtakiwa wa pili, Mombuli na Nyoni, wanakabiliwa na mashtaka ya kuwasilisha nyaraka za kumdanganya mwajiri na matumizi mabaya ya madaraka wawasilishe upya maombi ya dhamana Mahakama Kuu. Mapema jana washtakiwa hao walifikishwa viunga vya Mahakama ya Kisutu wakiwa saba.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Tehema, Joseph Makani, aliachiwa huru baada ya kuondolewa kwenye mashtaka hayo walipofutiwa kesi na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) juzi.

HABARI KITAIFA

# Hukumu 'Malkia wa Tembo' Februari 15

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imepanga kutoa hukumu ya kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kukutwa na meno ya tembo inayomkabili raia wa China, Yang Feng Glan maarufu kama 'malkia wa meno ya tembo' Februari 15, mwaka huu.

Mbali na mshtakiwa huyo, washtakiwa wengine ni Salvius Matembo na Phillemon Manase.

Uamuzi huo ulitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, aliyesikiliza kesi hiyo baada ya pande zote mbili jamhuri na utetezi kuwasilisha majumuisho ya mwisho.

Januari 28, mwaka huu mahakama hiyo ilipokea majumuisho ya mwisho kwamba washtakiwa wana hatia au la. Hakimu alisema mahakama yake itatoa hukumu Februari 15, mwaka huu. Awali upande wa Jamhuri uliita mashahidi 11 na utetezi watatu.

Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo uliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchini, Paul Kadushi na Wakili wa Serikali, Salim Msemo.

Msemo alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na kupangiwa tarehe ya kusikilizwa hukumu.

"Mahakama yangu itasoma hukumu dhidi ya washtakiwa Februari 15, mwaka huu" alisema Hakimu Shaidi.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo yenye thamani ya Sh.bilioni 13, kinyume cha sheria.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Januari Mosi, 2000 na Mei 22, 2014.

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa katika kipindi hicho walifanya biashara ya vipande 706 vya meno ya tembo vyenye uzito wa kilogramu 1889, vikiwa na thamani ya Sh.bilioni 5.4 bila kuwa na leseni kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

# Upinzani walia vifungu vinne muswada Sheria ya Vyama

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MUSWADA wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018, hatimaye umesomwa kwa mara ya pili bungeni, huku Kambi Rasmi ya Upinzani ikilia na vifungu vinne inavyodai ni hatari kwa ustawi wa siasa na demokrasia nchini.

Akisoma hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu muswada huo, Mbunge wa Bunda Mjini (Chadema), Esther Bulaya, aliwataka wabunge wote bila kujali itikadi za vyama vyao, kukataa kuunga mkono alichodai uonevu kwa kufuta vipengele vyote kandamizi ndani ya muswada huo.

Bulaya alisema kambi inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 3(c) ambacho kinatoa mamlaka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kuingilia mfumo wa uchaguzi ndani ya vyama kwa kuwa kinapunguza uhuru wa vyama kufanya uchaguzi bila shinikizo kutoka katika Ofisi ya Msajili.

"Kwa sababu hiyo, Kambi ya Upinzani inapendekeza kifungu hicho kifutwe na badala yake msajili awe na jukumu la kukuza demokrasia na utawala bora ndani na miongoni mwa vyama vya siasa," Bulaya alisema.

Kambi hiyo pia ilishauri kifungu chote cha 5A na vipengele vyake kifutwe pamoja na kifungu chote cha 8C kwa kuwa vimejaa adhabu, faini na vifungo kwa atakayekiuka masharti ya vifungu hivyo.

Alisema wanavitafsiri kama ni hila mbaya ya kuvizuia vyama vya upinzani kushirikiana na vyama rafiki katika kueneza itikadi zao na kupata mafunzo ya namna bora ya kuendesha siasa za kistaarabu na kushamiri.

Bulaya alisema kifungu kingine wanachopendekeza kufutwa ni 6A(3) ambacho kinaingilia utaratibu wa katiba za vyama kwa kutoa sharti kuwa mkutano mkuu au kamati kuu visikasimu madaraka yake.

Alisema kambi inaona huko ni kuingilia utaratibu wa kawaida wa vyama kwa mujibu wa katiba zao na kwamba yote yanaonekana kuwa na hila mbaya za kufifisha na kudumaza shughuli za vyama vya siasa.

**MAONI YA KAMATI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mohamed Mchengerwa, akiwasilisha maoni na ushauri wa kamati yake kuhusu muswada huo, alisema wamebaini kuna masuala ambayo endapo yasingefanyiwa marekebisho au kuondolewa, yangekwamisha utekelezaji wa sheria.

Miongoni mwa masuala hayo ni msajili kupewa mamlaka makubwa zaidi ya yale anayotakiwa kuwa nayo kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi, msajili kupewa jukumu la kuwa mshauri wa serikali kwa masuala ya demokrasia ya vyama vingi nchini, hatua ambayo ingeweza kuhatarisha demokrasia nchini kwa kumpa mtu mmoja kuamua hatma ya misingi ya katiba ya nchi.

"Pia, adhabu kubwa zenye kukosa uhalisia na ambazo zinakosa msingi wake chini ya sheria ya vyama vya siasa pamoja na sheria nyingine za nchi zinazopendekezwa kwa baadhi ya ibara za muswada huu zingekosa mantiki ya busara ya sheria inayopendekezwa," alisema na kuongeza:

INAENDELEA UK.8



Daktari bingwa wa magonjwa ya macho wa Hospitali ya Temeke, Husna Msangi, akitoa elimu ya utunzaji macho kwa wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) Kinyerezi, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kutoa huduma ya bure ya upimaji macho iliyotolewa kwa ushirikiano na Hospitali ya Macho ya Kimataifa (The International Eye Hospital). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa awapa maagizo mazito maofisa ustawi jamii

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka maofisa ustawi wa jamii katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa watekeleze majukumu yao kwa bidii, weledi, uadilifu na wasijihusishe na vitendo vya rushwa.

Amesema maofisa hao wanatakiwa watumie mbinu shirikishi ambazo zinahusisha jamii yenyewe na wataalamu ambao ni watoa huduma ngazi ya jamii ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo jana kwenye Mkutano wa Mwaka wa Kiutendaji wa Maofisa Ustawi wa Jamii katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, jijini Dodoma.

Waziri Mkuu aliwataka maofisa hao wahakikishe kwamba haki za msingi za makundi hayo zinapatikana kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo katika kutoa huduma ya taaluma yao.

Alisema taaluma ya ustawi wa jamii imepewa dhamana ya kuwa mlinzi wa mtoto, kumhudumia na kusimamia haki zake, hivyo amewataka wazuie na watokomeze aina zote za ukatili kwa watoto, wazee na wenye ulemavu.

Waziri Mkuu alisema jukumu hilo pia linahusisha watoto walio kwenye mazingira hatarishi na wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wazee, wanawake wasio na uwezo na watu wenye ulemavu.

Alisema pamoja na mafanikio makubwa ambayo serikali ya awamu ya tano imeyapata, ni muhimu wakaendelea kuongeza nguvu na weledi ili kutorudi nyuma katika kujenga msingi wa kuimarisha ustawi wa makundi maalumu.

Pia, Waziri Mkuu aliwaagiza maofisa hao wakasimamie utekelezaji wa mkakati wa mkono kwa mkono, familia kwa familia, kaya kwa kaya kupitia huduma ya kuzuia ukatili ngazi ya familia wenye lengo la kuzuia ukatili ndani ya familia ili ulete matokeo tarajiwa.

"Tambueni umuhimu wenu na kwamba jamii inawategemea kutekeleza majukumu yenu kikamilifu ili kupunguza matatizo ya kijamii kwa wale wenye uhitaji wakiwamo watoto, watu wenye ulemavu, wazee, familia zenye migogoro na kinamama wanaonyanyaswa na makundi mengine."

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amewashukuru wadau wa maendeleo kwa namna wanavyoshirikiana na serikali katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo likiwamo suala la uimarishaji wa huduma za ustawi wa jamii nchini.

Amesema anatambua mchango mkubwa kutoka kwa Shirika la UNICEF, USAID, UN WOMEN, UNFPA, John Snow Inc, Pact, HelpAge International, World Vision, Save the Children, Plan International na wengine wote ambao kwa namna moja au nyingine wameendelea kushirikiana na serikali kuinua kiwango cha utoaji huduma za ustawi wa jamii nchini.

"Ninapenda kuwahakikishia kuwa serikali iko tayari kufanya kazi pamoja nanyi, ili tuweze kufikia malengo ya maendeleo endelevu ifikapo 2030."

# BENKI YA STANBIC TANZANIA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2018

**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa | Robo Mwaka iliopita |
|---|---|---|---|
| | | 31-Des-18 | 30-Sep-18 |
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 14,823 | 11,112 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 132,530 | 99,793 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 69,089 | 70,385 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 119,874 | 63,622 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 35,743 | 29,049 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 76,591 | 41,349 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 193,426 | 254,473 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 674,165 | 642,609 |
| 12 | Mali Nyingine | 38,855 | 48,324 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 47,266 | 48,674 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,402,361** | **1,309,389** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 160,352 | 101,549 |
| 18 | Amana za Wateja | 851,380 | 828,443 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 49,124 | 36,729 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 58 | 145 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 26 | 26 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 37,608 | 38,126 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhisi Baina ya Benki na Mteja | 35,743 | 29,049 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 334 | 284 |
| 27 | Dhima Nyingine | 19,741 | 32,569 |
| 28 | Madeni | 18,502 | 18,654 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,172,866** | **1,085,574** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **229,495** | **223,814** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 7,390 | 7,390 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 75,487 | 75,487 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 131,372 | 131,372 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 17,092 | 10,669 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | -1,845 | -1,103 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **229,495** | **223,814** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 584,279 | 722,120 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 56,488 | 50,676 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 38,007 | 36,327 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16.4% | 17.1% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.9% | 7.5% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 79.9% | 79.2% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 53.3% | 54.1% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 74.8% | 79.3% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 4.1% | -2.4% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 7.1% | -2.2% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2018

**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | TAARIFA | Robo ya Mwaka sasa 31-Des-18 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Des-17 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Des-18 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Des-17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 23,350 | 24,204 | 93,005 | 90,824 |
| 2 | Gharama za Riba | 2,839 | 3,899 | 10,588 | 13,921 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **20,511** | **20,305** | **82,417** | **76,902** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 922 | 729 | 6,696 | 4,563 |
| | **Mapato baada ya tengo katika mikopo** | 19,589 | 19,576 | 75,720 | 72,340 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **13,436** | **12,804** | **52,745** | **58,680** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 8,140 | 7,747 | 28,492 | 34,017 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 5,175 | 4,865 | 23,482 | 21,854 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 121 | 192 | 771 | 2,809 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | **23,569** | **24,960** | **102,683** | **101,339** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 12,966 | 13,831 | 53,919 | 52,913 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 4,244 | 4,405 | 16,186 | 14,644 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 6,359 | 6,725 | 32,577 | 33,782 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **9,456** | **7,419** | **25,783** | **29,680** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 3,033 | 2,377 | 8,691 | 10,367 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **6,423** | **5,042** | **17,092** | **19,314** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| | i) Mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | -2,682 | 3,658 | -3,437 | 8,363 |
| | ii) Kodi ya mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | 805 | -1,098 | 1,039 | -2,509 |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **4,546** | **7,603** | **14,694** | **25,168** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 539 | 559 | 539 | 559 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.9 | 0.7 | 2.3 | 2.6 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 9 | 9 | 9 | 9 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.5% | 0.4% | 1.3% | 1.6% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.9% | 2.3% | 7.7% | 9.1% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 64.1% | 67.4% | 70.5% | 67.8% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.0% | 2.0% | 8.0% | 8.1% |

*Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho*

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018

**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | TAARIFA | Robo Mwaka ya sasa 31-Des-18 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Des-18 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Des-17 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **6,423** | **4,359** | **17,092** | 19,314 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 3,827 | 3,842 | 7,669 | 7,155 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | -73,491 | -16,254 | -181,222 | 26,035 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | -218 | 3 | -215 | 2,462 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 100,828 | -40,976 | 100,430 | 112,866 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 62,343 | 22,622 | 146,377 | -196,690 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | -13,383 | 8,663 | 8,842 | 6,187 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 8,880 | -2,888 | 5,960 | 3,655 |
| | - Kodi Iliyolipwa | -87 | -1,882 | -9,886 | -11,557 |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **95,121** | **-22,512** | **95,047** | **-30,574** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | -1,690 | -677 | -3,590 | -9,541 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 165 | 20 | 248 | 3,033 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **-1,525** | **-657** | **-3,342** | **-6,507** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | -153 | 438 | 18,502 | - |
| | Mengineyo (bainisha) | -742 | -1,869 | -13,452 | 5,909 |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **-895** | **-1,431** | **5,050** | **5,909** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 92,701 | -24,600 | 96,755 | -31,173 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 174,526 | 199,126 | 170,472 | 201,645 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 267,227 | 174,526 | 267,227 | 170,472 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2018

**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mabadiliko thamani katika amana zinazouzika | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| | **Salio la mwanzo wa mwaka** | 7,390 | 75,487 | 131,372 | 2,496 | 4,648 | 4,463 | 225,855 |
| | Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 17,092 | - | - | - | 17,092 |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | -2,398 | -2,398 |
| | Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | 1,424 | -2,496 | 1,072 | - | - |
| | Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | -11,256 | - | - | 202 | -11,054 |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **7,390** | **75,487** | **138,632** | **-** | **5,719** | **2,267** | **229,495** |
| 2 | **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| | **Salio la mwanzo wa mwaka** | 7,390 | 75,487 | 113,140 | - | 5,138 | -521 | 200,633 |
| | Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 19,314 | - | - | - | 19,314 |
| | Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 5,854 | 5,854 |
| | Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| | Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| | Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | -2,006 | 2,496 | -490 | - | 0 |
| | Mengineyo | - | - | 925 | - | - | -871 | 54 |
| | **Salio la mwisho wa mwaka** | **7,390** | **75,487** | **131,372** | **2,496** | **4,648** | **4,463** | **225,855** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2018**

Katika kuaanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Ken Cockerill **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | | 28-Jan-19 |
| Lydia Kokugonza **(Mkuu wa Fedha)** | | 28-Jan-19 |
| Jonathan Ngoma **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | | 28-Jan-19 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1. Prof. Marck Mwandosya **(Mwenyekiti wa bodi)** | | 28-Jan-19 |
| 2. Nada Margwe **(Mjumbe wa bodi)** | | 28-Jan-19 |

Stanbic Bank Moving Forward™
A member of Standard Bank Group

# TANGAZO

## DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2015

## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES

### (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| No. | Item/Transaction | Charges/Fees TZS | USD |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Current Accounts** | | |
| a) | Required Minimum balance | 0 | 0 |
| b) | Monthly Service/Management Uhuru Banking | FREE | FREE |
| c) | Monthly Service/Management Private banking PAYT | 29,500 | 17.70 |
| d) | Monthly Service/Management Fees Private banking Bundle | 53,100 | 31.86 |
| e) | Monthly Service/Management Fees Biashara Direct segment | 22,000 | 13.20 |
| f) | Monthly Service/Management Fees Sole propriator segment | 15,000 | 10.62 |
| g) | Monthly Service/Management Fees SME banking segment | 35,400 | 21.24 |
| h) | Monthly Service/Management Fees Commercial banking segment | 64,900 | 38.94 |
| i) | Monthly Service/Management Fees Non commercial Entities | FREE | FREE |
| j) | Monthly Service/Management Fees Corparate Banking | 33,040 | 12.98 |
| k) | Over the counter withdrawal fee(per segment and price option) | TZS 3,894 for amounts below 20M, 0.15% of value for amount above 20M max 118,000 | For FCY withdrawals - 1.18% min 7.08, Maximum US$300 |
| l) | ATM withdrawal fee own ATM Private banking | 900 | 0.60 |
| m) | ATM withdrawal fee own ATM Uhuru Banking | 950 | 0.83 |
| n) | ATM withdrawal fee other banks (local) Uhuru banking | 1,000 - 400,000 =2,800<br>400,001-above=4,000 | 1,000 - 400,000 =2.8<br>400,001-above=4 |
| o) | ATM withdrawal fee other banks (local) Private Banking | 1,000 - 50,000 =1,200<br>50,001 - 200,000 = 1,900<br>200,001 - 400,000 = 2,800<br>400,001-above=4,000 | 1,000 - 50,000 =1.2<br>50,001 - 200,000 = 1.9<br>200,001 - 400,000 = 2.8<br>400,001-above=4 |
| p) | ATM withdrawal fee International | 8,000 | 5.00 |
| q) | ATM Mini Statement | 900 | 0.60 |
| r) | Interim Statement per page | 4,720 | 2.36 |
| s) | Periodic schedule statement | FREE | FREE |
| t) | Issue of cheque book | 413 per leaf | 0.36 per leaf |
| u) | Returned updaid Cheque( insuficient fund) | 100,000 | 60.00 |
| v) | Special Clearance | 47,200 | 28.32 |
| w) | Counter Cheque | 14,160 | 8.26 |
| x) | Stop Payment | 47,200 | 28.32 |
| y) | Salary processing to staff banking with STB(SFI) | 4,000 | 0.60 |
| z) | Salary processing to staff banking with STB(Manual) | 4,000 | 2.40 |
| aa) | Salary processing to staff banking with other bank(EFT) | 4,000 | 1.80 |
| ab) | Salary processing to staff banking with other bank(TISS) | 10,000 | Equivalent of 10 000 |
| ac) | Standing Order to 3rd partywithin stanbic | 4,720 | 2.36 |
| ad) | Standing Order to other banks local | 33,040 | 17.70 |
| ae) | Standing Order own account | FREE | FREE |
| af) | Balance enquiry (Over the counter) | 4,720 | 2.36 |
| ag) | ATM card issuance | FREE | FREE |
| ah) | ATM card replacement/Renewal | 25,000 | 15.00 |
| ai) | Unarranged Overdraft | 100,000 | 60.00 |
| aj) | Overdrawn Account interest charge | 36% | 21% |
| ak) | Interbank Transfer Normal | 3,000 | 1.80 |
| al) | Interbank Transfer Express (TISS) | 10,000 | Equivalent of 10 000 |
| am) | Interbank Transfer | 33,040 | 17.70 |
| an) | Bill Payments through non branch channels( E channel) | FREE | FREE |
| ao) | Deposit fee | FREE | FREE |
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 50,000 | 100.00 |
| b) | Monthly service fee (if balance breach minimum balance required) | 2,000 | 1.18 |
| c) | Interim statement | FREE | FREE |
| d) | Account closure | FREE | FREE |
| **3.0** | **Electronic banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | FREE | FREE |
| b) | Internet transfers within own accounts STB | FREE | FREE |
| c) | Internet transfers 3rd party transfer STB | 1,000 | 0.60 |
| d) | Internet transfers other banks normal(EFT) | 2,000 | 1.20 |
| e) | Internet transfers other banks express(TISS) | 8,000 | Equivalent of 8 000 |
| f) | Bank to wallet Private Banking | 1,000 - 50,000 =1500<br>50,001 - 200,000 = 2000<br>200,001 - 300,000 = 2500<br>300,001-500,000=3000<br>500,000-1,000,000=3,500 | Equivalent |
| g) | Bank to wallet Uhuru Banking | 1,000 - 25,000 =1500<br>25,001 - 100,000 = 2000<br>100,001 - 250,000 = 2500<br>250,001-500,000=3000<br>500,000-1,000,000=3,500 | Equivalent |
| h) | Balance and statement | FREE | FREE |
| i) | Air time top up | FREE | FREE |
| j) | SMS Banking | FREE | FREE |
| k) | Till to bank | 1.5% of the amount | 1.5% of the amount |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowlwdge and information

Signed by:

| | | |
|---|---|---|
| **Chief Executive Officer** | **K. Cockerill** | ........................................ |
| **Head, Personal and Bussiness Banking** | **Ndadzungira, Brian B** | ........................................ |
| | | ........................................ |

| No. | Item/Transaction | Charges/Fees TZS | USD |
|---|---|---|---|
| **4.0** | **Foreign Exchange Transactions** | | |
| a) | Purchase/Sale of TC's ttransactions over the counter | N/A | 1.475% min 43.66 |
| b) | Purchase of foreign cheque | 1.18% of the amount min 100 000, | 1.18% of the amount min 59, Max 236 |
| c) | Telegraphic transfer Inward | N/A | 0.25% Min $11 Max $35 |
| d) | Telegraphic transfer Outward | N/A | 0.295%. Min $50, Max 150 |
| e) | Telegraphic transfer Outward( For TT done from TZS a<br>TISS outward | N/A<br>10,000 | $59<br>10 000 Equivalent |
| | | 0.826 | |
| f) | TISS inward | FREE | FREE |
| g) | Cancellation of TT/Recall of funds | N/A | $75 |
| **5.0** | **Personal Loan** | | |
| a) | Processing/ Arrangement/ Appraisal fee | | |
| | (i) Personal Loans | 2.00% | 2.00% |
| | (ii) Overdrafts | 2% of the facility min 100 000. | 2% of the facility min $100 |
| | (iii) Mortgage Finance | 1.18% | 1.18% |
| | (iv) Asset Finance | 1.18% | 1.18% |
| b) | Early repayment | 3.0% | 3.0% |
| | Valuation fees | As per valuer | As per valuer |
| **6.0** | **Other Disclosures (Viambatanisho Vinginevyo)** | | |
| | Base/Prime Lending Rate | 21% | 9% |
| | Maximu spread over Base/Prime lending rate | 4.5% | 2% |
| **7.0** | **Deposit Rate (*subject to change from time to time*)** | | |
| | a) Fixed Deposits | | |
| | **TZS** | **+1BN** | **+1M** |
| | 1month | 1.25% | 0.05% |
| | 3months | 1.45% | 0.10% |
| | 6months | 1.90% | 0.15% |
| | 9months | 2.80% | 0.20% |
| | 12months | 3.70% | 0.25% |
| | b) Savings Account | 3.00% | 0.20% |
| | c) Current Account | Nil | Nil |
| **8.0** | **Trade Finance** | | |
| | a) Letters of Credit/Guarantee | | |
| | Establishment Fee - per quarter | Nil | 1% on establishment per quarter and part thereoff min $300 |
| | b) Documentary collection( clean bill) | Nil | $150 |

**Stanbic Bank** Moving Forward™

A member of Standard Bank Group

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Waziri Mkuu kwa Ustawi wa jamii ni la msingi

**KATIKA** toleo letu la leo tumeripoti kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka maafisa Ustawi wa Jamii katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa watekeleze majukumu yao kwa bidii, weledi, uadilifu na wasijihusishe na vitendo vya rushwa.

Amesema maafisa hao wanatakiwa watumie mbinu shirikishi ambazo zinahusisha jamii yenyewe na wataalamu ambao ni watoa huduma ngazi ya jamii ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo jana kwenye Mkutano wa Mwaka wa Kiutendaji wa Maafisa Ustawi wa Jamii katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, jijini Dodoma.

Waziri Mkuu aliwataka maafisa hao wahakikishe kwamba haki za msingi za makundi hayo zinapatikana kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo katika kutoa huduma ya taaluma yao.

Alisema taaluma ya Ustawi wa Jamii imepewa dhamana ya kuwa mlinzi wa mtoto, kumhudumia na kusimamia haki zake, hivyo amewataka wazuie na watokomeze aina zote za ukatili kwa watoto, wazee na wenye ulemavu.

Alisema jukumu hilo pia linahusisha watoto waliopo kwenye mazingira hatarishi na wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wazee, wanawake wasio na uwezo na watu wenye ulemavu.

Alisema pamoja na mafanikio makubwa ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imeyapata, ni muhimu wakaendelea kuongeza nguvu na weledi ili kutorudi nyuma katika kujenga msingi wa kuimarisha ustawi wa makundi maalumu.

Hivi sasa changamoto kubwa katika jamii yetu ni ukiukwaji mkubwa wa haki za makundi ya watoto, wanawake na walemavu ukiwamo wa vitendo vya ukatili dhidi yao ambavyo vinatokea kila uchao. Itakumbukwa jinsi wanawake na watoto wa kike wanavyoathiriwa na vitendo vya udhalilishaji na ukatili vikiwamo kubakwa, vipigo kukeketwa, ndoa na mimba za utotoni, kukosa haki za msingi kama elimu, afya, kumiliki na kurithi.

Vitendo hivi kimsingi, vinawakosesha fursa muhimu za maisha na kubaki wakihangaika katika umaskini mkubwa.

Watu wenye ulemavu nao wamekuwa wakikosa haki zao za msingi kutokana na kunyanyapaliwa bila sababu za msingi. Kundi hili pia limekuwa mwathirika wa vitendo vya ukatili yakiwamo mauaji dhidi ya wenye ulemavu wa ngozi.

Aidha, tumeshuhudia wazee wakipata mahangaiko kutokana na kukosa msaada wa baadhi ya ndugu na jamaa zao na wakati mwingine jamii kuwapuuza. Ni kundi hili ambalo limekuwa likiathiriwa na mauaji kwa madai kuwa ni washirikina, kwa madai yasiyothibitika kuwa ni wachawi.

Kwa hmaelekezo aliyoyatoa waziri Mkuu kwa maafisa ustawi jamii ni ya msingi kwa sababu wabao wajibu wa kuilinda jamii kwa namna mbalimbali hususan makundi tajwa kwa lengo la kutokomeza aina zote za ukatili kwa dhidi yao.

Sisi tunaamini kwamba maafisa hao kila mmoja akiwajibika kwa nafasi yake, ukubwa wa changamoto zilizopo zitapungua kwa kiwango likubwa kama si kuisha kabisa.

Wadau ambao wamekuwa wakishirikiana na serikali katika kusukuma mbele maendeleo ikiwamo suala la uimarishaji wa huduma za ustawi wa jamii.

Waziri Mkuu amewashukuru wadau wa maendeleo kwa namna wanavyoshirikiana na Serikali katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo likiwamo suala la uimarishaji wa huduma za ustawi wa jamii nchini, na tunaamini kuwa wataendelea kuzidi kuunga mkono jitihada hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

BUSARA

**TUSIWE SEHEMU YA MATATIZO**
**KERO NA MATATIZO YOYOTE YANATAKIWA KUTATULIWA KWA HARAKA NA SIYO KUENDELEA KUYAFUGA. TUAZIMIE KUZIONDOA KERO ZILIZOPO NA ZILE ZITAKAZOKUJA, TUKIEPUKA SISI WENYEWE KUWA SEHEMU YA MATATIZO HAYO. TUSIWE VIKWAZO KATIKA SULUHISHO. MARIDHIANO NI DAWA.** NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kamati za Bunge zimefanya jambo la maana, lenye tija

**HIVI** karibuni Kamati tatu za Kudumu za Bunge zilipokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu miswada mitano ya sheria.

Miswada hiyo ni pamoja wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2018.

Mwingine ni wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2018.

Vikao vilianza Januari 16 kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ambayo ilipokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa mwaka 2018.

Nayo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilikutana na wadau wake ili kusikiliza na kupokea Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa mwaka 2018 na Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini wa mwaka 2018.

Kwa upande wake Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilipokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa mwaka 2018 kwa siku mbili mfululizo kuanzia Januari 17 na 18.

Januari 19 na 20 kamati hiyo pia ilipokea na kusikiliza maoni ya wawakilishi kutoka kila chama cha siasa kilichosajiliwa nchini, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018.

Hapa ndipo ninapotaka kuzungumzia zaidi, hasa uamuzi wa kuita wadau wa siasa kujadili muswada huo, ambao ulipigiwa kelele na wadau hao kuwa haufai na kutaka wananchi waukatae.

Lakini hatua zilizochukuliwa za kuwaalika wadau kutoa maoni yao ni njia nzuri inayolenga kupata mwafaka kuliko kuacha malalamiko yakiendelea.

Ikumbukwe kuwa mara nyingi meza ya mazungumza husaidia kuwafanya watu kukaa pamoja na hatimaye kupata mwafaka kwa kile wanachotofautiana.

Inawezekana muswada huo una upungufu wake na mazuri yake, hivyo kitendo cha kuwaita wadau baada ya kuwapo kwa malalamiko, ili kukaa pamoja na kuujadili ni hatua nzuri ya kuondoa malalamiko.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alikaririwa na vyombo vya habari akisema kwamba licha ya muswada huo kupingwa, lakini una mambo mazuri.

Alitoa mfano wa kuzuia kuwapo kwa vikundi vya ulinzi vya vijana katika vyama vya siasa, kwamba hatua hiyo inaweza kusaidia kuepusha vurugu, ambazo zimekuwa zikidaiwa kusababishwa na vikundi hivyo katika mikutano.

Kwa mtazamo wangu alichosema Dk. Ally kuhusu kuondolewa kwa vikundi hivyo ni hatua nzuri ambayo inaweza kuondoa tuhuma ambazo zimekuwa zikivikabili.

Ninasema hivyo, kwa sababu imekuwa ni jambo la kawaida kukuta vijana wakiwamo wa Blue Guard, Green Guard na Red Brigade kukumbwa na tuhuma za kuanzisha vurugu katika mikutano ya vyama vya siasa.

Vijana ni chachu ya maendeleo kwenye vyama vya siasa, kwa sababu wana nguvu na ni wepesi, lakini wanapotumiwa vibaya ni hatari kwao na kwa vyama vyao.

Baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiwatumia vibaya ili kutimiza malengo yao na hivyo kujikuta katika lawama kama hizo za kujihusisha kwenye vurugu.

Kama nilivyosema, hatua ya kuwaita wadau katika meza ya mazungumzo itasaidia kumaliza changamoto ambazo zilijitokeza hasa lawama zilizokuwa zikitolewa na baadhi ya wanasiasa kuhusu muswada huo.

Vijana ni muhimu katika siasa, lakini watumike vizuri, wasigeuzwe kuwa madaraja ya baadhi ya wanasiasa na kujikuta wakiumizana wenyewe kwa sababu ya itikadi za kisiasa.

Lakini pia hatua ya kuondoa vikundi hivyo ninaiona ni muhimu sana wakati huu, ambako kuna mihemko ya kisiasa ambayo imekuwa ikisababisha watu kuumizana kwa sababu tu hawako chama kimoja.

**TANGAZO**


# Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFAZA FEDHA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 Desemba 2018
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Desemba 2018 | Robo Mwaka iliyopita 30 Septemba 2018 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 849 | 1,443 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,586 | 8,333 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 49,500 | 52,530 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 9,883 | 2,562 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 4,737 | 28,859 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 69,901 | 69,084 |
| 12 | Mali Nyingine | 8,593 | 9,821 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 855 | 388 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **155,904** | **173,020** |
| B. | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 45,050 | 56,847 |
| 18 | Amana za Wateja | 68,764 | 71,688 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 5,040 | 5,017 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 44 | 35 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,197 | 2,533 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 360 | 338 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **121,455** | **136,458** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **34,449** | **36,562** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 1,630 | 3,584 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 7,606 | 7,674 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,346 | 2,308 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,367 | 1,496 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **34,449** | **36,562** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 5,906 | 5,164 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 4,967 | 7,921 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,332 | 1,984 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22.10% | 21.13% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.97% | 11.15% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 59.93% | 53.21% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 44.84% | 39.93% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80.48% | 88.12% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -11.01% | -4.10% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -9.89% | -2.91% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZIKWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 Desember 2018
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa 31 Desemba 2018 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 Desemba 2017 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 Desemba 2018 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 Desemba 2017 |
| Faida baada ya mabadiliko | - | - | 36,212 | - | - | - | 36,212 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 15,574 | 15,574 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (26,118) | - | - | - | (26,118) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 48,843 | (48,843) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (680) | - | 680 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (1,502) | - | - | 1,670 | 167 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **463,424** | **-** | **27,217** | **19,209** | **733,460** |
| **BANK** | | | | | | | |
| **Mwaka wa sasa-31/12/2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **442,494** | **-** | **26,796** | **15,135** | **708,035** |
| -Salio la mwanzo wa mwaka | 65,296 | 158,314 | 442,494 | - | 26,796 | 15,135 | 708,035 |
| -Maabadiliko ya mwanzo wa mwaka | - | - | (28,051) | - | - | - | (28,051) |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 65,296 | 158,314 | 414,443 | - | 26,796 | 15,135 | 679,984 |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 70,182 | - | - | - | 70,182 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 8,059 | 8,059 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (13,059) | - | - | - | (13,059) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (3,642) | - | 3,642 | - | - |
| Mengineyo | - | - | 203 | - | - | (203) | (0) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **468,127** | **-** | **30,438** | **22,991** | **745,166** |
| Mwaka uliopita-31/12/2017 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | | | | | | | |
| -Salio la mwanzo wa mwaka | 65,296 | 158,314 | 399,784 | 48,533 | 26,537 | (187) | 698,278 |
| -Maabadiliko ya mwanzo wa mwaka | - | - | (10,561) | - | - | - | (10,561) |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 65,296 | 158,314 | 389,223 | 48,533 | 26,537 | (187) | 687,717 |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 30,809 | - | - | - | 30,809 |
| -Mabadiliko ya faida mwaka uliopita | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida baada ya mabadiliko | - | - | 30,809 | - | - | - | 30,809 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 15,628 | 15,628 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (26,118) | - | - | - | (26,118) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 48,533 | (48,533) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (259) | - | 259 | - | - |
| Mengineyo | - | - | 306 | - | - | (306) | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **65,296** | **158,314** | **442,494** | **-** | **26,796** | **15,135** | **708,035** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2018**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

# MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES 2019

| TRANSACTION | AMOUNT (TZS) SAVINGS ACCOUNT | CURRENT ACCOUNT |
|---|---|---|
| Required minimum opening balance | 20,000 | 100,000 |
| Monthly s ervice fee | 1,888 | Corporate 17,700<br>Personal/SME 15,340 |
| Electronic statement | Free | Free |
| Adhoc statement | 1,999 Per Month | 1,999 Per Month |
| Withdrawal charges | 3,540 | 4,720 |
| Cash deposit charge | Free | Free |
| Issuance of TemboCard | Free | - |
| Closing account | 5,900 | 23,600 |
| Periodic schedule statement | - | Free |
| E-statement monthly | Free | Free |
| Cheque book (per leaf) | | 472 |
| Dishonoured cheque | | 1.2% min 177,000 max 354,000 |
| Cash payment to 3rd party (if there is no cheque list) | | 2,360 |
| Bulk cash depos it (for s mall denomination) | | 0.24% min 2,360 |
| Stop payment order (for already issued cheque) | | 1.2% min 59,000, max 354,000 |
| Standing orders (within the same bank) | | 1,999 |
| Salary handling | | 1,999 |
| TRA collection | | Free |

| | AMOUNT (TZS) |
|---|---|
| **EFT** | |
| Outward transfers | 1,950 |
| Inward transfers | 4,720 |
| **ATM TRANSACTION** | |
| (a) International cards | |
| Issue of TemboCard (faulty) | Free |
| Replacement of TemboCard (lost) | 23,600 |
| (b) ATM Withdrawals | |
| Within the same bank (on us) | 1,200 |
| To other banks ATM (on others) | 3,540 |
| ATM mini statement | 299 |
| **SIMBANKING** | |
| Balance inquiry | 354 |
| Transfer to own account | 699 |
| Transfer to third party account | 829 |
| Mini statement | 295 |
| Mobile Top up | Free |
| Bills payment | Free |
| Transfer to MNOs; | |
| up to - 200,000 | 2,499 |
| 200,001 - 500,000 | 4,199 |
| 500,001 - 1,000,000 | 6,399 |
| **RATES** | |
| Deposits up to TZS 1 Billion | |
| 3 Months | 1.5% - 3.5% |
| 6 Months | 2% - 4% |
| 9 Months | 2.5% - 4.5% |
| 12 Months | 3% - 5% |
| 24 Months | 4% - 5% |
| 36 Months (Thamani) | 5% |
| Prime lending rate (declining) | 19% |

| | AMOUNT (TZS) |
|---|---|
| **TISS** | |
| Outward transfers | 11,800 |
| Inward transfers | Free |
| **INTERNET BANKING** | |
| Balance inquiry | Free |
| Payments | Free |
| Fund transfer to own and third party | 899 |

CRDB BANK
The bank that listens



## Introducing New CRDB Bank Internet Banking

BANKING HAS NEVER BEEN SO SIMPLE.

SIMPLE AND INTUITIVE EXPERIENCE ACROSS ALL DEVICES

STATE OF THE ART SECURITY

SO SIMPLE AS WITHDRAWING CASH AT ATM

- Pay your bills
- Make payment to other banks: TISS & EFT
- Make international payments: SWIFT
- Make bulk payments to accounts & mobile wallets
- Make forex payments
- Make Government payments through GEPG
- Transfer money

crdbbank.co.tz | CRDBBankPlc | @crdbbankplc | CRDBBankPlc | CRDBBankPlc | CRDBBankPlc

Ukurasa 20



**MNANGAGWA AKIEPUKE 'KIKOMBE CHA MUGABE'**

## MAKALA:
Tanzania imechelewa kuwa na akiba ya dhahabu, ichangamke





Ukurasa 18

## KIMATAIFA:



**Trump, Erdogan waigawa Syria**

Ukurasa 19


# siasa

JUMATANO JANUARI 30, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


# Tshisekedi atazimudu changamoto 'zilizowasumbua' Mobutu, Kabila?




Rais Felix Tshisekedi wa DRC

**Na Mashaka Mgeta**

JANUARI 24, mwaka huu, utawala wa takribani miaka 17 wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Joseph Kabila ulifikia ukomo wake, baada ya kuapishwa kwa Rais Felix Tshisekedi.

Tshisekedi alishinda kwa kupata kura zaidi ya milioni saba zikiwa sawa na asilimia 38.57, wakati mshindani wake wa karibu, Martine Fayulu wa muungano wa Lamuka wenye kumaanisha 'amka', aki-

ENDELEA UK 16



**Sanga atamani serikali za mitaa ziongozwe na wanawake 2019**

Ukurasa 14

UCHAMBUZI

# Sanga atamani serikali za mitaa ziongozwe na wanawake 2019

- Wapewe mkakati, mafunzo maalum ili waingie maeneo mbalimbali ya madaraka
- Mitaa na vijiji ndiko kwenye ukatili wa kijinsia
- Idadi ya wanawake wanaoteuliwa Awamu ya Tano, imepungua kulinganisha na iliyopita

**Na Salome Kitomari**

UNAPOWATAJA manguri wa habari na wanawake waliosimama kupambania haki za wanawake na watoto Tanzania, jina la Edda Sanga, litakuwa miongoni mwao.

Hiyo inatokana na ukweli kuwa alipeperusha vyema bendera ya Chama cha Waandishi Wanawake Tanzania (Tamwa) wakati wa uongozi wake.

Akiwa miongoni mwa waanzilishi 12 wa Tamwa mwaka 1987, alihakikisha uwakilishi wa mwanamke katika nyanja mbalimbali unakuwepo ikiwamo kwenye siasa, serikalini na ngazi zote kutoka mtaa hadi taifa.

Mara zote na takribani katika ngazi zote za uchaguzi, ule wa serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu, Sanga kupitia Tamwa na mashirika mengine alipaza sauti ya kushawishi wanawake wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Alipaza sauti wagombee nafasi hizo ndani ya vyama na taasisi zao, si kwa sababu ya jinsia yao bali sifa walizonazo.

Aidha, alisimama kuhakikisha wanawake wanachaguliwa na hata kuteuliwa katika nafasi za kimaamuzi ambazo zinawezesha moja kwa moja sauti au mambo ya mwanamke na mtoto wa kike kusikika.

Kadhalika, kwa upande wa vyombo vya habari, alipigania kuhakikisha habari za wanawake zinaandikwa kwa muundo ambao si wa kuwadhalilisha kutokana na maumbile au sura yao na kuhakikisha kwenye habari zinazoandikwa kuna sauti ya mwanamke.

Januari 11, mwaka huu, Sanga amehitimisha safari yake ya utumishi ndani ya Tamwa kama Mkurugenzi Mtendaji, baada ya kushika nafasi hiyo kwa miaka mitatu huku akiwa na mengi ya kujivunia ambayo yamesaidia kubadilisha fikra za jamii dhidi ya wanawake na watoto.

Aidha, kwa upande wa vyombo vya habari, amesaidia kutambua umuhimu wa sauti za wanawake kusikika ikiwa ni pamoja na kuwaamini walio na sifa na kuwapa nafasi za kimaamuzi.

Baada ya kukabidhi kijiti kwa Rose Ruben, ambaye ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa sasa wa Tamwa, Sanga aliongea na Nipashe katika mahojiano maalum.

Nipashe lilitaka kujua maoni yake kuhusiana na uchaguzi wa serikali za mitaa wa Agosti mwaka huu na uchaguzi mkuu wa Oktoba mwakani.

Sanga anasema wakati Tamwa inaanzishwa jamii ilikuwa haielewi kuwa wanawake wana mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi na wanahitaji kuthaminiwa, lakini pia harakati au majukumu yao yahesabike kwenye suala zima la maendeleo ya jamii.

"Ukweli ni kwamba wakati huo tulitafuta kupata waandishi wa habari wanawake wengi zaidi, ili habari ziweze kuandikwa kwa jicho la jinsia na hata kwa namna ambavyo tunapenda kuziona...tunaona mabadiliko makubwa kwa kwa sasa, habari za wanawake zinaripotiwa," anasema.



Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Tamwa, Edda Sanga. **PICHA: MTANDAO**

> "Kwa Kikwete ilikuwa rahisi sana kutokana na eneo analotoka, mfumo dume haupo kwa kiasi kikubwa na ndiyo maana aliteua wanawake wengi kwenye nafasi za uongozi,"

**UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA**

Sanga anasema Tamwa ilivyoanzishwa mwaka 1987 iliangalia uongozi wa mwanamke, namna gani anaweza kuingia kwenye nafasi za uongozi ili kuleta tofauti kwenye uongozi na masuala yanayopiganiwa yaweze kupata muafaka mapema kwa jicho la mwanamke.

"Kama ambavyo tuliwaomba 2015 tupate wanawake wengi inavyowezekana, ambao wanajitambua na ambao watapewa mkakati na mafunzo maalum ya kuwawezesha kuingia katika maeneo mbalimbali ya madaraka," anasema.

Anabainisha kwamba kuna watu wanaweza kujitambua kuwa wana uwezo wa kuwa viongozi lakini kama hawajaandaliwa vyema kuelewa watashindwa kusimamia hoja zenye kuleta mabadiliko chanya.

"Tunaposema ni kiongozi wa kike maana yake ni nini, anajenga au anabeba ajenda gani huko anakotafuta uongozi... ni lazima apate ajenda ya kwenda nayo na si vyema kutaka uongozi kwa sababu kuna nafasi hiyo," anasema na kuongeza:

"Ni vyema unapokwenda kwenye nafasi ya uongozi ujue unataka kufanya nini...upewe ajenda za kwenda kusimamia...bahati mbaya sana tuna tabia ya kutokujifanyia tathmini ili kujua unakwenda kwa malengo gani."

Nguri huyu wa habari anasema mtu anapokwenda na malengo na kufanikiwa kupata anachokitafuta ni rahisi kutathmini malengo aliyoenda nayo kama yamefikiwa na kwa kiasi gani, changamoto zilizopo, pale aliposhindwa na sababu za kushindwa.

Sanga ambaye alikuwa Mtangazaji wa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), anasema ni vyema wagombea au wenye nia wakapata mafunzo ya uongozi kwenye suala zima la jinsia.

"Na hayo yafanywe na mashirika mbalimbali ya kutetea haki za wanawake na vyombo vya habari," anasema.

Kwa upande huu, gwiji huyu anasema waandishi wa habari wana nafasi kubwa ya kuandika makala ambazo zitawasaidia wanawake kujitambua, kujiamini, kuelewa masuala ya jinsia ni yapi na wanawezaje kuyachukua kama ajenda na kuitafsiri.

"Kuna kazi kubwa sana ya kufanya, kama wanawake na kama waandishi wa habari na tunayo nafasi kubwa ya kusaidia kwa kuwatambua wanaotaka kuingia, tuwaulize ni ajenda gani wanachukua na uongozi maana yake ni kuonyesha njia au ni zaidi ya hapo," anasisitiza.

**UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA**

Sanga anasema anatamani kazi kubwa itafanyike mwaka huu, ili wanawake wengi waingie kwenye uongozi wa serikali za mitaa.

"Ngazi ya serikali za mitaa na vijiji ndiko kwenye ukatili wa kijinsia, masuala mazito ya wanawake ya kilimo, ardhi, shule na mengine...si sawa kuangalia kwenye ubunge tu bali hata kwa wenyeviti na madiwani," anasema.

Anabainisha ngazi za chini ndizo zitakazoleta matokeo mazuri mbele ya safari kwa kuwa wanawake wengi watakuwa wamekwenda na ajenda muhimu zenye kutatua kero za mwanamke na mtoto wa kike na hivyo kutokomeza ukatili dhidi yao.

**MWANAMKE NA UONGOZI**

Anasema tangu uingie madarakani uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, idadi ya wanawake wanaoteuliwa kwenye nafasi mbalimbali imepungua kwa kiasi kikubwa, ikilinganishwa na awamu zilizopita.

"Iko tofauti ya uongozi wa Rais John Magufuli na wa awamu wa nne ya Jakaya Kikwete, kwa kuwa anakotoka Kikwete ni mrengo wa kinamama yaani kina shangazi, lakini Dk. Magufuli ametoka kwenye mfumo dume ambao umejikita kweli kweli," anasema wakati akijibu swali la waandishi kuhusu anavyouona uongozi wa sasa na uliopita katika uteuzi wa wanawake.

"Mfumo dume umejikita katika baadhi ya makabila na mojawapo ni huko anakotoka rais wetu... wakati mwingine inakuwa vigumu kumthamini na kumwamini mwanamke kwa sababu ya malezi, makuzi na kurithishana kizazi kimoja hadi kingine," anaongeza.

Hata hivyo, gwiji huyu anasema anaamini hadi Rais Magufuli atakapomaliza kipindi chake cha uongozi, atakuwa amepata mabadiliko fulani.

"Kwa Kikwete ilikuwa rahisi sana kutokana na eneo analotoka, mfumo dume haupo kwa kiasi kikubwa na ndiyo maana aliteua wanawake wengi kwenye nafasi za uongozi," anasema.

Sanga anasema Watanzania au wanawake wangependa kuona katika utawala huu wanawake wanapewa nafasi za uongozi kutokana na sifa na uwezo wao wa kazi.



Rais Paul Kagame wa Rwanda (kushoto), Rais Yoweri Museveni wa Uganda (katikati) na Rais Pierre Nkurunziza wa Burundi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Viongozi nchi Maziwa Makuu wakoleza 'mchezo mchafu'

**Na Ani Jozeni**

VIONGOZI wa nchi za Maziwa Makuu ambao wanakutanishwa na eneo la Mashariki ya Congo (DRC) lililosheheni machafuko wanatuhumiwa kuendeleza michezo michafu ya kulea makundi ya kivita, kudhoofishana, ili kukaza uzi wa mamlaka katika kila mojawapo ya nchi hizo.

Nchi hizo ni Congo (DRC), Burundi, Rwanda na Uganda, kuwa kuna hali ya kutokutakiana mema ambayo inaweza isibadilike kwa lolote kwa utawala mpya kuingia nchini DRC, kwani tofauti hizo ni za msingi katika maeneo tofauti.

Ndiyo picha inayotokeza katika tafiti za wachambuzi wa Ufaransa, kuhusu mzozo unaoendelea kati ya Rais Paul Kagame na Pierre Nkurunziza.

Mtafiti Gerard Prunier, mkongwe wa siasa za eneo hilo la Afrika na hivi sasa mkurugenzi wa kituo cha Ufaransa cha utafiti kuhusu Ethiopia jijini Addis Ababa, anasema kuwa ziko nchi za pembeni zinazochangia hali hiyo, ikiwemo Sudan, Sudan Kusini na Afrika ya Kati.

Anasema Ufaransa imesaidia kuondoa hali ya vita vya wenyewe kwa wenyewe huko Afrika ya Kati, vilivyosaidia kulea makundi ya kivita na kihalifu hasa yanayoilenga Uganda, kama LRA (Lord's Resistance Army) aliyosema ni kundi la kihalifu na lenye njozi za 'siku za mwisho,' ADF (Allied Democratic Front) ambayo inaungwa mkono na Rais Omar al-Bashir wa Sudan, halafu M-23.

Prunier anabainisha kuwa kundi la M-23 ambalo ni la Rais Kagame linalomsaidia kudhibiti usalama eneo la Mashariki ya DRC katika eneo ambalo Rwanda ina maslahi ya kutafuta madini na kuyauza kwa njia inazojua yenyewe, sasa limehamishia maskani yake Sudan Kusini.

Kinachoshangaza katika mazingira ya sasa ni kuongezeka kwa mashambulizi nchini Uganda ya kundi la ADF kutokea Congo, huku Rais Kabila kwa muda wote akiwa anaangalia tu bila kuchukua hatua yoyote madhubuti.

Watafiti wa Ufaransa wanasema hali hiyo haishangazi kwani DRC na Uganda zinagombea utajiri wa mafuta chini ya Ziwa Albert ambalo ni mpaka wa nchi hizo mbili.

> Kuuawa kwa Rais Ndadaye kulirudisha nyuma mazungumzo ya amani Burundi na kuingiza nchi katika vita ya wazi ya wenyewe kwa wenyewe, ambako Nkurunziza alifaulu kuunda kundi la kijeshi lenye upenyo katika sehemu kubwa ya jamii.

Moja ya maeneo waliotilia umuhimu katika uchambuzi huo uliochapishwa katika jarida la 'Le Monde Diplomatique' (mapitio ya hali ya kidiplomasia duniani) wachambuzi hao wanaashiria kuwa vita vya hapa na pale katika kila mojawapo ya nchi hizo inasaidia utawala wa nchi jirani unaokosolewa na nchi hiyo.

Hali hiyo ni ya wazi katika ugomvi kati ya Rwanda na Burundi kwani kwa mujibu wa watafiti hao, Rais Kagame anataka kuweka utawala unaofanana na ule wa Rwanda wa kundi la kijeshi la RPF (Rwanda Patriotic Front) ambalo liko madarakani.

Kikwazo ni kuwa Burundi haina ugomvi wa kina wa kimbari kama ule wa Rwanda, zinatofautiana.

Suala la kuwepo kwa utawala nchini Burundi unaofanana na ule wa Rwanda yaani kwa msingi wake kijamii, yaani kimbari na hivyo kisiasa, ni kuwa Rais Kagame hana mpango wa kuondoka madarakani, hali ambayo kama ilivyo Uganda inasababisha mikwaruzano inayoongezeka na makundi ya upinzani. Isitoshe, kama ilivyo kwa Rais Nkurunziza na Rais Yoweri Museveni wa Uganda, kuacha aliyekuwa Rais Joseph Kabila nchini DRC, kuwepo kwa hatari ya vita ya hapa na pale kunawezesha hatua za kiusalama kuongezeka, na hivyo kusaidia kuzuia wapinzani kujieleza au kuwafikia wananchi kwa upana au utulivu unaohitajiwa. Ni kuishi kivita, ikibidi.

Kutokana na ugomvi wake na Kagame, Nkurunziza anaonekana kutumia kila nafasi anayopata kuonyesha upinzani dhidi yake kama wa kikabila, yaani ki-Tutsi, jambo ambalo siyo sahihi kwani Burundi imepitia hatua nyingi za kujenga madaraja na mahusiano ya kina kati ya makundi hayo kijamii, licha ya kuwa mzizi wa fitina za kikabila haujawahi kuondolewa moja kwa moja.

Tofauti mojawapo kati ya nchi hizo mbili ni kuwa mazungumzo ya Arusha yalifikia amani kwa Burundi mwaka 2005, miaka 12 baada ya askari wa kitutsi kumuua Rais Melchior Ndadaye aliyechaguliwa kwa wingi wa kura Julai 1993. Haikuwa hivyo kwa upande wa Rwanda, katu.

Mazungumzo ya Rwanda yalipofikia hitaji la kuundwa kwa serikali ya pamoja huku vikosi vya kundi la RPF vikisonga mbele maeneo mengi hasa ya mashambani nchini humo, ndipo mauaji ya Rais Ndadaye yalitokea, na kuharibu kabisa mwelekeo wa majadiliano ya Rwanda.

Badala ya kuelekea muafaka na RPF, sehemu kubwa ya walioshika dola nchini Rwanda, wakiongozwa na washirika wa karibu wa Rais Juvenal Habyarimana walibadili gia na kutaka 'suluhisho kamili' la tatizo hilo (la Watutsi kutaka mamlaka ya nchi ili wawarudishe Wahutu ambao kimsingi walikuwa wanajitawala Rwanda, utumwani kama Burundi).

Ndiyo hapo ukazuka mpango wa mauaji ya kimbari, yakitumia zaidi kundi la mgambo la Interahamwe, chini ya taasisi ya Akazu, kutokea Ikulu.

Kuuawa kwa Rais Ndadaye kulirudisha nyuma mazungumzo ya amani Burundi na kuingiza nchi katika vita ya wazi ya wenyewe kwa wenyewe, ambako Nkurunziza alifaulu kuunda kundi la kijeshi lenye upenyo katika sehemu kubwa ya jamii.

Kutokana na hali hiyo vyama vya siasa vya jadi vilianza kujifia, na vingine vyenye silaha za hapa na pale vikashindwa kustahimili kishindo cha CNDD-FDD (jina linalohusisha mapambano ya siasa ya kidemokrasia, na uwepo wa harakati ya kijeshi kama sehemu ya chama hicho).

Matokeo yake ni kuwa chama hicho kimeunda mazingira tofauti ya kisiasa nchini humo yanayotegemea sana maamuzi ya Rais Nkurunziza ili kuweka sehemu zote za jamii sawa, kutokana na migongano mingi hasa wingi wa watu na uhaba wa ardhi kote.

Tatizo hilo linaendana pia na hali ya siasa nchini Rwanda ambako wa sehemu kubwa Rais Kagame ni tumaini la wengi kuweka nchi hiyo katika amani, kwani akiondolewa halafu 'masanduku' ya kilichotokea awali yaanze kufunguliwa patakuwa hapakaliki.

Ni mazingira hayo pia yanayoisibu Uganda, kwani kuna tawala za kifalme takriban 10 zenye migongano na wivu nani mwenye ardhi ipi, wabunge, vyeo serikalini, n.k.

Licha ya kuwa kuna harakati kubwa zaidi hasa kwa upande wa vijana (wa kizazi kipya) kutaka kuondoka madarakani Rais Museveni, kazi hiyo si rahisi kama ilivyo nchini Sudan ambako maandamano yamekwama.

Watafiti hao wanasema ni hapo alikwama Kabila, kuwa hakuwa ni tegemeo la kuwepo amani kati ya makundi tofauti, hasha.

MAKALA

Inatoka Uk.13

# Tshisekedi atazimudu changamoto ‘zilizowasumbua’ Mobutu, Kabila?

tangazwa kupata kura milioni 6.3 (sawa na asilimia 34.38) ya kura zilizopigwa.

Wakati waliokuwa wapinzani hao wakichuana kwa karibu, aliyekuwa mgombea kupitia muungano wa People’s Party for Reconstruction and Democracy (PPRD) wa chama tawala, Waziri wa Mambo ya Ndani wa zamani wa DRC, Emmanuel Ramazani Shadary, alipata kura zaidi ya milioni 4.3 (sawa na asilimia 23.84).

Tukio la kihistoria la kukabidhiana madaraka kwa njia ya amani lililofanyika jijini Kinshasa, lilikuwa la kwanza tangu Taifa hilo kupata uhuru wake Juni 30, 1960.

Baada ya uhuru, ilikubaliwa kuwa Patrice Lumumba awe Waziri Mkuu na Joseph Kasa Vubu akiwa rais wa kwanza wa nchi hiyo.

Hata hivyo, baada ya muda mfupi wa kuwapo kwake madarakani, alitofautiana na wenzake kuhusu mzozo wa kisiasa kwenye mikoa ya Katanga iliyokuwa inataka kujitawala na kusababisha (Lumumba) kuuawa mwaka 1961.

Mwaka 1965, Mobutu Sese Seko Kuku Ngbendu wa Zabanga ambaye alikuwa Mkuu wa Majeshi, aliongoza mapinduzi ya kijeshi na kuitawala nchi hiyo kwa miaka 32.

Wakati wa uongozi wake, nchi ya DRC ilijulikana kama Zaire huku raia wake wakiitwa Wazaire.

Wakati wa uongozi wa Mobutu, Laurent-Desire Kabila alianza harakati za kumwondoa madarakani kupitia kundi la waasi, alipata msaada wa nchi jirani na mwaka 1997, alifanikiwa kuingia madarakani baada ya kumwangusha Mobutu.

Akiwa madarakani, Kabila alibadili jina la nchi hiyo kutoka Zaire kuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)).

Mwaka 2001, aliuawa baada ya kupigwa risasi na mlinzi wake, kisha mtoto wake, Joseph Kabila (aliyekabidhi madaraka karibuni) akapewa uongozi wa nchi hiyo.

Tshisekedi anayekiongoza chama cha United for Democracy and Social Progress (UDSP) anakuwa Rais wa tano wa DRC, akishikilia pia rekodi ya kiongozi wa kwanza kuingia madarakani kwa mara ya kwanza kupitia sanduku la kura.

Tume Huru ya Uchaguzi nchini humo (CENI), ilimtangaza Tshisekedi kuwa mshindi wa Uchaguzi Mkuu uliofanyika Desemba 30, mwaka jana na baadaye kuidhinishwa na Mahakama ya Katiba `iliyotupilia mbali’ shauri la kupinga ushindi huo kutoka kwa aliyekuwa mgombea wa nafasi hiyo, Martin Fayulu

**HOTUBA**

Akilihutubia taifa kwa mara ya mwisho akiwa Rais, Kabila aliwataka raia wa DRC kumuunga mkono Rais Tshisekedi, na kuelezea furaha yake kwa ushindi huo kwenda upinzani na kwamba atakuwa tayari kumsaidia kwa kadri itakavyohitajika, kufanikisha ajenda za maendeleo ya nchi hiyo.

Wakati Kabila akitoa kauli hiyo, taarifa nyingine zilienea DRC zikidai kuwa wawili hao (Kabila na Tshisekedi) walikubaliana ili kufanikisha hujuma za ‘kuchakachua’ matokeo ya Urais, lakini

> “Hoja inayoibuka hapo ni ikiwa Rais Tshisekedi ataikumbuka historia hiyo na kuweka mfumo bora wa kugawa madaraka ili kupunguza kama si kuziba mianya ya kuibuka kwa vikundi vya waasi hasa vyenye malengo kama vilivyopita?



Kiongozi wa upinzani anayedai kupokwa ushindi, Martine Fayulu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Rais wa zamani wa DRC, Mobutu Sese Seko Kuku Ngbendu wa Zabanga

pande za viongozi hao ziliyakana madai hayo.

Wadau mbalimbali likiwamo Kanisa Katoliki lenye ushawishi mkubwa nchini DRC, walielezea wazi Rais Tshisekedi ‘amewekwa madarakani’ na Kabila ili kulinda maslahi binafsi na washirika wake.

**CHANGAMOTO ZINAZOMKABILI TSHISEKEDI**

Ushindi alioupata Rais Tshisekedi haukupokewa kwa shangwe ama kuaminiwa na wengi ndani na nje ya DRC. Wapo waliojitokeza na kuupinga hadharani huku wengine wakiukosoa na kuutilia shaka, hivyo kuomba kura zihesabiwe upya.

Miongoni mwa hao watatajwa baadaye kwenye makala haya, lakini kwa jumla hali hiyo haikuashiria ‘jambo jema’ kwa mshindi huyo ambaye hakutarajiwa na wengi.

Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Ujerumani (DW), Andrea Schmidt, alikaririwa na kituo cha redio ya shirika hilo akisema halitokuwa jukumu rahisi (kwa Rais Tshisekedi) ikizingatiwa kwamba ushindi wake aliupata kutokana na msaada wa utawala wa Rais wa zamani, Kabila.



Rais aliyekabidhi madaraka hivi karibuni, Joseph Kabila.

DW ikamkariri Schmidt akisema, “Wakongomani wamevunjwa moyo na uchaguzi wa hadaa ya kidemokrasia katika nchi yao... hata hivyo ni wachache tu wanaounga mkono wito wa maandamano alioutoa Fayulu... Wanataka hatimaye kuona maendeleo, umoja na amani baada ya miongo kadhaa ya mizozo.”

Anasema, raia wa DRC wamechoshwa kuona watumishi wa Serikali wakizidi kutajirika wakati watoto wadogo wakifa kwa maradhi ya kipindupindu, watu wakisumbuliwa na njaa, wakilazimika kuwakimbia wanamgambo, wanawake kubakwa, miongoni mwa kadhia nyingine.

**NAMNA YA ‘KUGAWA’ MADARAKA**

Ukubwa wa DRC, ubovu wa miundombinu, urahisi wa vikundi vya waasi wanaojificha misituni ni baadhi ya mambo yanayotarajiwa kuwa ‘pasua kichwa’ kwa Rais Tshisekedi katika kukabiliana na usalama wa uhakika nchini humo.

Tangu utawala wa awamu ya kwanza, DRC imeshindwa kufanikisha ujenzi wa barabara imara za kuunganisha mikoa na hivyo kuifanya ifikike kwa shida. Sehemu ya barabara hizo zinatajwa kupitia kwenye misitu mikubwa inayotumiwa na waasi.

Vikundi vya waasi kuweka makazi yao kwenye ardhi ya DRC limekuwa jambo linalopigiwa kelele na takribani viongozi wote wanaoingia madarakani, huku nchi za jirani hususani Uganda na Rwanda zikinyooshewa vidole na kutuhumiwa kwa kuvifadhili.

Zipo sababu kadha wa kadha zinazochochea kushamiri kwa vikundi vya waasi vinavyohatarisha amani ya DRC, kati ya hizo ni uporaji na utoroshaji wa madini ya aina tofauti yanayopatikana nchini humo.

Mbali na vikundi hivyo, wapo waasi wengine wanaoibuka katika DRC wakitaka kuchukua madaraka, ama kujigawia maeneo ya utawala katika taifa hilo.

**KUEPUKA UASI**

Ikumbukwe kwamba muda mfupi baada ya uhuru, DRC ilikuwa katika ‘machafuko ya kisiasa’ yaliyohusisha vikosi vya kijeshi vilivyoyateka majimbo mawili kisha kumuingiza madarakani Mobutu.

Kwa upande wake, Mabotu naye hakuondoka madarakani kwa uchaguzi wa kidemokrasia, isipokuwa ‘kufurumushwa’ na vikosi vya waasi vilivyoongozwa na Kabila Baba.

Ilikuwa katikati ya miaka ya 1990, Kabila Baba aliporejea DRC (wakati huo Zaire) na kuwa kiongozi kikundi cha Alliance of Democratic Forces for the Liberation of Congo-Zaire.

Kikundi hicho kilipinga utawala wa kidikteta wa Mobutu, kikiwatumia zaidi Watutsi kutokea Mashariki mwa DRC, wakaelekea hadi Magharibi hadi kuingia jijini Kinshasa na hivyo kumlazimu Mobutu aikimbie nchi hiyo Mei, 17, 1997.

Kabila akajitangaza kuwa Rais na kuibadili jina kutoka Zaire kuwa DRC.

Uasi kama huo ulizidi kushuhudiwa DRC hata baada ya kifo cha Kabila Baba. Vurugu za kisiasa zilizowahi kutokea DRC zilisababisha mgawanyiko uliotishia kuligawa taifa hilo kiutawala.

Hali ilisababisha Rais (mstaafu) Joseph Kabila kukubali wazo la kuwaleta pamoja wapinzani na asasi za kijamii, ili kupata suluhu ya amani, na kutokana na hali hiyo, Kabila aliwateua Makamu wa Rais wanne na kuwapa majukumu tofauti katika (iliyokuwa) serikali yake.

Walioteuliwa walikuwa Azarias Ruberwa aliyeiongoza Rally for Congolese Democracy (RCD), Arthur Z’ahidi Ngoma, Abdoulaye Yerodia Ndombasi wa Party for Reconstruction and Democracy (PPRD) na Jean-Pierre Bemba wa Movement for the Liberation of Congo (MLC).

Hoja inayoibuka hapo ni ikiwa Rais Tshisekedi ataikumbuka historia hiyo na kuweka mfumo bora wa kugawa madaraka ili kupunguza kama si kuziba mianya ya kuibuka kwa vikundi vya waasi hasa vyenye malengo kama vilivyopita?

**USHIRIKIANO**

Ushirikiano wa wadau wa ndani hasa wapinzani na jumuiya za kikanda kwa kadri ya uanachama wa DRC ni jambo jingine linalomkabili Rais Tshisekedi katika utawala wake.

Hali hiyo inatokana na baadhi ya jumuiya hizo, kutoa matamko ya awali yenye kutilia shaka, kukosa na kutoyakubali matokeo yaliyompa ushindi.

Kwa mfano, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), baada ya matokeo kutangazwa, iliitisha kikao cha dharura jijini Addis Ababa, Ethiopia kujadili matokeo ya uchaguzi huo.

SADC yenye washirika wawili wakubwa wa DRC kama Afrika Kusini na Angola, ilitoa wito wa kuhesabiwa upya kwa kura za urais, lakini rai hiyo ikapingwa na Afrika Kusini na Zambia.

Pia, SADC ilipendekeza kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa vikiwamo vyama vilivyowateua Shadary na Fayulu kuwania kiti hicho.

Januari 13 mwaka huu, Mkutano wa Kimataifa wa Ukanda wa Maziwa Makuu (CIRGL) wenye wanachama 12, ulielezea hisia hasi za

Inaendelea Uk. 18



Dk. Kizza Besigye, kiongozi wa upinzani nchini Uganda. **PICHA: MTANDAO**

## Viongozi wa upinzani barani Afrika waliojitangazia ushindi mapema

**MARTIN FAYULU**

ALIIOMBA Mahakama ya Katiba ya DRC, kuyafuta matokeo ya uchaguzi.

Fayulu aliyakataa matokeo ya uchaguzi wa urais wa Desemba 30, 2018, ambapo alishika nafasi ya pili akiwa ameshindwa na Felix Tshisekedi, mgombea mwingine wa upinzani.

Fayulu akafungua kesi kwenye Mahakama ya Katiba akiitaka iufute ushindi wa Tshisekedi. Lakini Mahakama ikasema madai yake si ‘halali.’ Fayulu alipata asilimia 34.8 ya kura, huku Tshisekedi akishinda kwa asilimia 38.57.

**MAURICE KAMTO WA CAMEROON**

Maurice Kamto, mgombea wa upinzani wa muungano wa MRC na FDP, alijitangaza mshindi wa uchaguzi wa urais uliofanyika Jumapili ya Oktoba 7, 2018.

Ni mmoja kati ya wagombea saba walioshindana na kiongozi wa muda mrefu wa Cameroon, Paul Biya ambaye amekuwa madarakani kwa miaka 36.

“Ninamtaka Rais Biya ahakikishe kipindi cha amani cha mpito na kuepuka matukio yanayoweza kuwa mabaya,” alisema Kamto.

**NELSON CHAMISA, ‘RAIS HALALI’ WA ZIMBABWE**

Kiongozi mdogo wa upinzani nchini Zimbabwe, Nelson Chamisa, aliupinga ushindi wa Rais Emmerson Mnangagwa katika uchaguzi wa kwanza wa urais baada ya utawala wa Robert Mugabe uliofanyika Julai 30, 2018.

Alijitangaza mshindi wa urais katika sherehe za kujiapisha.

**SOUMAILA CISSE AYAKATAA MATOKEO NCHINI MALI**

Soumaila Cisse wa Mali hakwenda mbali hadi kuandaa hafla ya kujiapisha, lakini alizungumzia kuhusu pengo la uongozi nchini Mali, baada ya mpinzani wake Ibrahim Boubacar Keita kuchukua madaraka.

Agosti 20, Mahakama ya Katiba ilimtangaza Keita mshindi wa uchaguzi, baada ya kupata asilimia 67 ya kura katika duru ya pili ya uchaguzi.

**‘RAIS WA WANANCHI’ WA KENYA**

• Apeana mkono na mwenye mamlaka

JANUARI 20, 2018, Raila Odinga, mpinzani mkuu wa Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta, alijiapisha mwenyewe kama ‘rais wa wananchi.’

Alisusia marudio ya uchaguzi wa Oktoba 2017, baada ya kushinda kesi mahakamani kuhusu uhalali wa uchaguzi wa kwanza.

Huku mazingira ya baada ya uchaguzi yakiwa ya wasiwasi, Machi 2018, Odinga na Kenyatta walitangaza kupeana mkono wa maridhiano na kusameheana.

**JEAN PING: ‘NITATUMIA MAMLAKA MLIYOWEKEZA KWANGU’**

Miaka miwili baada ya uchaguzi wa urais Agosti 2016, kiongozi wa upinzani wa Gabon, Jean Ping bado anaendelea kuonyesha azma yake.

Agosti 2018, alithibitisha nia yake ya kuendelea kupambana. Awali Ping alielekeza matumaini yake katika uchunguzi wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi. Hata hivyo, kesi hiyo ilifungwa. Haikukidhi vigezo vya uchunguzi.

BESIGYE WA UGANDA, Mpinzani wa muda mrefu

Februari 2016, Kizza Besigye aligombea urais kwa mara ya nne dhidi ya kiongozi wa muda mrefu wa Uganda, Yoweri Museveni.

Wakati Museveni alipotangazwa mshindi, Besigye alijiapisha mwenyewe katika sherehe mbadala.

Alikamatwa na kufunguliwa mashtaka ya uhaini, lakini aliachiwa huru wiki chache baadaye.

**ETIENNE TSHISEKEDI; ‘MSHINDI’ WA MARA MBILI WA DRC**

Mwaka 2006 na 2011, Etienne Tshisekedi, kiongozi wa chama cha UDPS katika DRC, alidai kumshinda Rais Joseph Kabila.

Alionekana kama mmoja wa wapinzani wakuu wa Kabila, akiwa na matumaini ya kugombea katika uchaguzi mwingine.

Alifariki mwaka 2017, baada ya kuugua ambapo mtoto wake Felix Tshesekedi ambaye ni rais wa sasa wa DRC, alichukua uongozi wa chama.

**DW**

# Tanzania imechelewa kuwa na akiba ya dhahabu, ichangamke

**Na Gaudensia Mngumi**

THAMANI ya fedha ya taifa lolote zama hizi inashikiliwa na uwezo wa nchi kuuza bidhaa na huduma kwenye masoko ya nje.

Hivyo kama taifa linauza kwa wingi bidhaa na huduma zenye thamani kubwa, inamaanisha hifadhi ya fedha za kigeni inakuwa kubwa.

Vivyo hivyo, taifa linalouza dhahabu kwa wingi kwenye soko la nje linakuwa na sarafu yenye thamani na nguvu kubwa zaidi.

Ni kwa sababu dhahabu ni madini ya thamani tena yasiyobadilika yakitumiwa na wafalme, mataifa na madola mbalimbali hata kabla na baada ya ujio wa Masiha Yesu Kristo.

Wiki iliyopita Rais John Magufuli, akizungumza na wadau wa madini jijini Dar es Salaam, anasema Tanzania ni taifa lenye dhahabu kwa wingi lakini, halijanufaika kikamilifu na dhahabu hivyo ni wakati wa kuanzisha akiba ya dhahabu ya taifa.

Dhahabu hiyo inatunzwa na Benki Kuu (BoT). Lakini pia pamoja na kuwa na dhahabu anashauri taifa kuanzisha senta (vituo) au magulio ya kuuza madini na kuachana na utaratibu wa sasa ambao haulisaidii taifa kupata mapato.

Kwa mfano aliambiwa kuwa biashara ya vito kama almasi hufanywa hotelini au popote sirini kwani hakuna vituo vya kuuza madini hayo kwenye migodi yanapozalishwa.

Lakini pia hakuna gulio au senta ya kuuza Tanzanite Mererani, hivyo husafirishwa kutoka machimboni wilayani Simanjiro hadi Arusha kwenye gulio na katika njia hiyo madini hupotea hapo katikati.

Masuala hayo ni muhimu kwa taifa kuwa na akiba ya dhahabu BoT na magulio ya kuuzia madini na vito.

Licha ya Tanzania kuwa nchi ya tatu Afrika kwa kuzalisha dhahabu kwa wingi ikitanguliwa na Afrika Kusini na Ghana imechelewa mno kuanzisha hifadhi hiyo kwani madini hayo ni muhimu kiuchumi na mlinzi mkuu wa sarafu ya nchi, kwa sababu huipa nguvu zaidi na kuiimarisha.

Dhahabu ni kitu cha thamani kwa uchumi na hata kisiasa. Mathalani historia inaeleza kuwa dhahabu ilitumiwa na wafalme kama Mfalme Suleimani ambaye aliitumia kujenga mahekalu huko Yerusalemu.

Utajiri mkubwa wa dhahabu unatajwa katika Dola la Zimbabwe ikitoka katika mji wa Sofala.

Aidha, ndani ya kitabu cha Zaburi (45.9) kinataja Malkia aliyesimama mkono wa kuume wa Mungu akiwa amevaa dhahabu ya Ophiri.

Hivyo, dhahabu inahusishwa na utukufu, utajiri, mamlaka na nguvu kiuchumi na kisiasa.



Mmoja wa wachimbaji madini (kushoto), aliyeshiriki kwenye mkutano wa Rais John Magufuli (kulia), alipokutana na wadau wa madini nchini hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

> "Ni vyema kushirikiana na benki iliyotambulishwa rasmi na kukubalika na wanaushirika ili kuwakopesha... kupitia benki inawezekana kupata taarifa sahihi za kiasi cha madini kinachozalishwa, kinachouzwa kwenye soko rasmi (gulioni au kwenye senta) na baadaye kuuzwa nje ya nchi,"

**AKIBA YA DHAHABU BoT**

Kuanzisha akiba ya dhahabu ni jambo lililokubaliwa zaidi ya miaka 53 iliyopita kwani Sheria ya kuanzisha Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya mwaka 1966 (imeshafanyiwa marekebisho), inaipa benki hiyo uwezo wa kuanzisha hifadhi ya dhahabu.

Ibara ya 53 inasema, BoT ina jukumu la kuweka akiba (reserve) iwe ya fedha na hata kuweka akiba ya dhahabu.

Hivyo, akiba ya dhahabu ndani ya benki ni mtaji, mali isiyobadilika thamani, sarafu imara na mlinzi wa uchumi.

Ni Madini yanayoweza kutumiwa kukopa au kupata fedha za kigeni wakati wowote uchumi unapoteterека. Kwa hiyo kuwa na hifadhi ya dhahabu ni kuwa na 'pesa juu ya pesa.'

**MSOMI**

Akizungumzia suala la kuanzishwa akiba ya dhahabu BoT, Profesa Michael Ndanshau wa Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) anasema:

"Ni vizuri kwamba BoT itaanza kununua dhahabu sasa...niseme kwa hili tumechelewa sana na ilikuwa kosa kusitisha ununuzi wa dhahabu uliokuwa ukifanyika hapo awali."

Profesa Ndanshau anaona kama taifa limechelewa kujenga hifadhi ya madini hayo na kwamba ni jambo lililokuwa lifanyike siku nyingi kama ambavyo sheria inaelekeza.

Kwa Tanzania inaweza kununua dhahabu kwa njia mbili, kwa mfano kuichukua kutoka kwenye kampuni za wazalishaji ambao kama BoT na serikali zitaridhia walipe dhahabu halisi badala ya mrabaha.

Kwa hiyo, wataalamu wakokotoe na kupata thamani ya fedha ya mrabaha ili ilinganishwe na dhahabu halisi itakayopelekwa BoT badala ya hundi kupelekwa hazina.

Kadhalika, BoT inaweza kununua madini hayo kutoka kwa wachimbaji wadogo wanaozalisha dhahabu sehemu na maeneo mbalimbali.

**VITO /MADINI MENGINE**

Profesa huyu wa uchumi anasema kwa upande wa madini mengine kama vito mfano Tanzanite, almasi na rubi ni vyema kuanzisha senta au magulio maalumu ya wachimbaji katika sehemu zinazotengwa maalumu katika maeneo yenye migodi, kama Rais anavyoelekeza.

"Ni lazima kuwe na usimamizi wa vyombo vya dola, polisi, wataalamu wa thamani wa madini, Mamlaka ya Mapato (TRA) na kuwe na matawi ya benki zitakazopenda kuingia kwenye biashara ya madini," anasema Profesa Ndanshau.

Anashauri wachimbaji wadogo wote wajiunge katika ushirika uliosajiliwa na wenye ofisi ili uruhusiwe kununua na kuuza madini katika gulio la madini.

"Ni vyema kushirikiana na benki iliyotambulishwa rasmi na kukubalika na wanaushirika ili kuwakopesha... kupitia benki inawezekana kupata taarifa sahihi za kiasi cha madini kinachozalishwa, kinachouzwa kwenye soko rasmi (gulioni au kwenye senta) na baadaye kuuzwa nje ya nchi," anasema.

Profesa Ndanshau anapendekeza kuwa mnunuzi au wanunuzi binafsi wanaotambulika, wenye leseni au ushirika, akieleza kuwa kuna tija zaidi iwapo biashara itafanyika kwa utaratibu huo.

Anafafanua kuwa ni jambo lenye tija iwapo ushirika unaoundwa kwa pamoja na wachimbaji wa madini pamoja na wanunuaji binafsi wataelekezwa kushirikiana na benki zilizopo na ambazo zitakubali, la msingi ni kupata garantii ya serikali au BoT waweze kukopa fedha ili kununua madini wakati wakisubiri kuyauza na kurejesha mkopo.

**AKIBA KUBWA YA DHAHABU**

Jarida la Forbes linataja mataifa yenye akiba kubwa ya dhahabu duniani kwa mwaka jana kwenye benki kuu zao kuwa ni Marekani inayoongoza kwa kuwa na tani 8,133.5.

Ya pili ni Ujerumani ina tani 3,381, nyingine ni Italia ikiwa imehifadhi tani 2,451.

Forbes inaitaja Ufaransa kuwa ni nchi ya nne duniani kwa kuwa na dhahabu nyingi kwenye benki kuu ikiweka tani 2,435.

China inafuatia kwa kuwa na tani 1, 797.5, Russia imo ikiwa na akiba ya tani 1, 460.47 , Uswisi pia imo ina tani 1,040, Japan ina akiba ya dhahabu ya tani 765.2 , Uholanzi ni miongini mwa mataifa yenye akiba kubwa ya madini hayo ikijikusanyia tani 612.5 na India haikuachwa nyuma, ina tani 557.5.

**AFRIKA**

Baadhi ya nchi zinazoongoza kuwa na akiba kubwa ya dhahabu ni Algeria tani 173.63, Afrika Kusini 125.28, Libya 116.64, Misri 76.29.

# Tshisekedi atazimudu changamoto 'zilizowasumbua' Mobutu, Kabila?

**Inatoka Uk.16/17**

kina kuhusu matokeo yaliyompa ushindi Rais Tshisekedi.

Januari 10, mwaka huu, Baraza Kuu la Maaskofu wa Kanisa Katoliki nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (CENCO) lilikosoa ushindi wa Tshisekedi na kusema matokeo hayo hayakuakisi uhalisia uliotolewa na waangalizi wake zaidi ya 40,000 'walioenea' nchini kote.

Kwa upande, mshindi wa pili katika uchaguzi huo, Martin Fayulu, alifungua shauri kwenye Mahakama ya Katiba akilalamikia 'kuchakachuliwa' kwa matokeo na kutaka yahesabiwe upya, lakini shauri hilo lilitupwa, akashindwa.

Je, ni kwa namna gani Rais Tshisekedi atayapa uzito masuala na hoja za makundi hayo na mengine mengi, ili mabadiliko waliyoyaonyesha baada ya kuidhinishwa kwake yasiwe yenye kukidhi msemo wa 'funika kombe mwanaharamu apite'?

**SHEREHE YA KUAPISHWA**

Kwa upande mwingine, ni desturi yenye kukuza ushirikiano wa kidiplomasia, kisiasa na kiuchumi pale viongozi wa nchi jirani wanapohudhuria hafla ya kuapishwa kwa viongozi wakuu wa mataifa jirani.

Lakini kuapishwa kwa Rais Tshisekedi hakukuwa hivyo. Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Ujerumani (DW), viongozi kutoka nchi nyingi za Afrika zikiwamo 'mahasimu' wa DRC, Uganda na Rwanda, hawakuhudhuria kuapishwa kwake.

Bila shaka changamoto zinazomkabili Rais Tshisekedi ni nyingi, zote zikijikita katika kukoleza maendeleo ya nchi hiyo na ustawi wa watu wake na zaidi ya yote, ni kuweka mazingira bora ya amani ya kweli kudumu DRC.

**Makala haya yameandikwa kwa masaada wa vyanzo mbalimbali na uchambuzi wa mwandishi anayepatikana katika namba +255 754 691540.**



Rais Donald Trump wa Marekani (kushoto), akiwa na Rais Recep Tayyip Erdogan wa Uturuki. **PICHA: MTANDAO**

# Trump, Erdogan waigawa Syria

## ■ wakimbizi kurudi eneo la Kaskazini

**Na Nimi Mweta**

MAHUSIANO kati ya Rais Donald Trump wa Marekani na Rais Recep Tayyip Erdogan wa Uturuki kuhusu Syria yamekuwa yakishangaza, huku wazungumzaji kuhusu suala hilo nchini Marekani wakioneka-na kudakia tu kinachosemwa hapa au pale, siyo mtazamo wa jumla.

Ndani ya utawala wa Rais Trump kulikuwa na shinikizo kubwa kuhusu mpango wake wa kuondoa vikosi vya Marekani nchini Syria, hata kufikia kujiuzulu kwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi, Jenerali Mstaafu James Matis.

Wakati huo huo, mshauri wa masuala ya usalama wa taifa, John Bolton alifanya juhudi kuhakikisha kuwa Marekani inaondoka kwa mpangilio, ikiwezekana pole pole zaidi ya inavyotazamiwa, na tofauti na alivyoelekeza Trump, wa vikosi kuondolewa huko kwa haraka.

Kilichowakwaza watu wengi (na hasa nchi zinazoshirikiana na Marekani katika kuzuia kupanuka kwa wimbi la ISIS - Dola ya Kiislamu - huko Iraq na Syria) ni tangazo la Rais Trump kuwa ISIS imeshindwa, hivyo inafaa Marekani iondoe vikosi vyake.

Kuanzia wakati huo fikra halisi ya Trump imeelewe-ka, kuwa Uturuki inatosha kumalizia kazi ya kuifyekelea mbali ISIS katika eneo lililobaki Kaskazini ya Syria.

Ni fikra yenye vianzio vya mbali kuwa pale inapowezekana Marekani itumie vikosi au majeshi ya nchi jirani au zinazopakana nazo, hasa pale ambako wimbi hilo halitishii moja kwa moja usalama wa Marekani; kwa jumla hali ya Syria imepungua nguvu.

Moja ya vianzio vya kufanya uamuzi wa haraka kuondoa majeshi ya Marekani eneo hilo, ambao haukuanzia katika mikakati ya Jeshi la Marekani maeneo ya vita sehemu mbalimbali duniani, ni hisia kuwa ingefaa Uturuki iwe mlinzi wa eneo hilo, badala ya Marekani.

Licha ya kuwa Uturuki ni nchi yenye siasa za Kiislamu kwa kiwango fulani inaelewana na Marekani kwa njia tofauti na nchi kama Saudia, swahiba mwingine wa Marekani ambaye mifumo yake ya kijamii inalea moja kwa moja tishio la siasa kali.

Tofauti ni kuwa majeshi ya Syria yana hali ya ushabiki fulani kwa kundi la ISIS ambalo lilianzishwa kwa ushiriki wa taasisi za kijasusi za Uturuki na Saudia, pamoja na Marekani ili kuibana serikali ya 'siasa kali' ya ki-Shia nchini Irak, wakati wa waziri mkuu wa zamani Nur al-Maliki.

Ilibidi Rais Erdogan afanye mageuzi makubwa jeshini aweze kupambana na ISIS, 2017.

Hofu kubwa ya wachunguzi wa masuala ya usalama nchini Marekani ilikuwa ni kwamba Uturuki itachukua nafasi iliyoachwa wazi na kuondoka kwa vikosi vya Marekani ili kufutilia mbali makundi ya wa-Kurdi nchini Syria, ambayo ni mahasimu wakubwa wa utawala wa Uturuki kwa miaka mingi.

Yako makundi ya wa-Kurdi katika nchi kadhaa zinazopakana, hasa Iran, Iraq, Syria na Uturuki, na kote huko wanakandamizwa, wakitaka 'kurudi' katika nchi yao, yaani iwe moja waweze kujitawala, na si majimbo yanayofanana ya nchi kadhaa.

Ni mpangilio wa makundi tofauti ya ki-Kurdi, yana nguvu tofauti katika nchi hizo, ambako kwa Iraq wanatambuliwa na wana utawala wao wa ndani. Nchini Syria na Iran wamekandamizwa tu, na ni ngome ya upinzani Uturuki.

Inavyoelekea ni kuwa Rais Trump na Rais Erdogan wamefikia muafaka kuwa Uturuki haitageuza mitutu yake nchini Syria kuwangamiza wa-Kurdi ambao ni kama Marekani inawaacha solemba miongoni mwa maadui zao.

Kuna Uturuki kwa upande mmoja, serikali au majeshi ya serikali ya Syria kwa upande mwingine, na makundi ya siasa kali ya ISIS kwa upande uliobaki, hasa kama kundi hilo likifaulu kujikusanya kwa nguvu kutokana na kuondolewa kwa vikosi vya Marekani, kama wanavyohofia wengi tu katika Wizara ya Ulinzi nchini Marekani na sehemu isiyo ndogo ya washauri wa Trump katika Ikulu.

Ilibidi Rais Trump amuonye vikali Rais Erdogan kuwa akianza kuwashambulia wa-Kurdi basi Marekani 'itaangamiza uchumi wa Uturuki, ' na siyo kwa hatua za kijeshi.

Baadhi ya wakosoaji wa Trump walisema hakueleza atafanya nini hasa ili kuteketeza au kukwamisha uchumi wa Uturuki, lakini inaelekea Erdogan alielewa, na mwelekeo wake katika majadiliano na maofisa wa Marekani unachukua sura tofauti.

Moja ya mabadiliko ni kuwa Uturuki sasa inataka kuunda eneo la kuwalinda watu waliokimbia nchini humo kutokana na mashambulizi na mauaji ya kutisha ya ISIS kuanzia 2014 na 2015 wakati makundi ya mgambo wa Dola ya Kiislamu yakichipuka na kuenea kutoka nchi moja hadi nyingine.

Ni kama vile Erdogan anawaacha wa-Kurdi kuendelea kumiliki silaha zao na kuendesha siasa zao ndani ya mustakabali wa nchi ya Syria na mwelekeo wa vita inayoelekea ukingoni, mradi wasifanye shambulizi lolote ardhi ya Uturuki.

Licha ya kuwa Rais Trump hasemi hivyo, anaelekea kupendelea kushirikiana na Uturuki kuleta amani katika eneo la Kaskazini ya Syria na kuelekea Mashariki hadi mpaka wa Iraq (ambako ndiyo ISIS ilijikita katika nchi hizo mbili) kuliko kutegemea kundi hilo la wa-Kurdi.

Tofauti ni kuwa Uturuki ikiwa imeshika eneo hilo, kuna uwezekano wa mpango wa kimataifa unaohusisha nchi kadhaa kuwezesha hali ya vita kumalizika na kila kundi liwe na mipaka yake, pale ambapo nchi nyingine zinahusika, na siyo makundi tofauti dhidi ya serikali ya Syria.

Ndipo ukazuka mpango wa kuweka eneo salama kwa wakimbizi wa Syria kurudi makwao, ambako Uturuki inasema kiasi cha wakimbizi laki tatu tayari wamerudi Syria ya Kaskazini, na mamilioni wanangoja kurudi pia.

Endapo mpango huo utafanikiwa, utaigawa Syria katika maeneo mawili makubwa, moja likiwa chini ya utawala wa Rais Bashir al-Assad na jingine likiwa kimsingi chini ya Uturuki, kuzuia vita ya jeshi la Assad lisiwarudishe wakimbizi Uturuki, kuangamiza wa-Kurdi.

Ni kama ilivyokuwa nchini Iraq wakati wa utawala wa Rais Saddam Hussein baada ya uvamizi wa Kuwait kuiingiza Marekani kuondoa kadhia hiyo katika 'Operation Desert Storm' (tufani ya jangwani) halafu nchi ikawekwa katika maeneo matatu.

Kusini wanakokaa wa-Shia na Kaskazini ya wa-Kurdi yalikuwa yakijisimamia yenyewe huku utawala wa Saddam ukuzuiliwa kurusha ndege eneo hilo, kwa amri ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Nchi iliunganishwa tena baada ya uvamizi wa Marekani, wa 2003.

Matokeo hayo ya vita nchini Syria yanabadilisha kwa kiwango kikubwa walichoafikiana hapo mwanzo washauri wa karibu wa Trump, hasa mkwewe Jared Kishner na mwanamfalme wa Saudia, Mohamed bin Salman ambaye kimsingi alitaka Syria (yote) aachiwe Rais al-Bashir, kwa maana kuwa upinzani umeshindwa kubadili mfumo humo.

Siyo wazo linalokubalika kwa washirika wa Marekani na hata katika taasisi za kiserikali huko Washington, kuwa dikteta Assad aachiwe kila kitu na harakati za mabadiliko zitokomee mbali.

Kuwepo eneo salama la kurudi wakimbizi kunaweza kuweka jiwe la msingi la siasa za kidemokrasia, siyo kuupindua utawala huo kama makundi tofauti yalivyokuwa yanataka wakati wimbi la upinzani linapamba moto 2011.

Makundi hayo yalijimaliza katika tofauti zao, kuwa hakuna lenye uwezo wa kuiondoa serikali hiyo, halafu yakaleta balaa la ISIS.

MAKALA



Rais Emmerson Mnangagwa wa Zimbabwe..**PICHA: MTANDAO**

# Mnangagwa akiepuke 'kikombe cha Mugabe'

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA huu ulianza vibaya kwa utawala wa Rais Emmerson Mnangagwa, baada ya maandamano ya kupinga ongezeko maradufu la bei ya mafuta yaliyoitishwa na chama cha wafanyakazi nchini humo.

Ongezeko hilo la mafuta likachangia sababu ya kupanda kwa gharama za maisha, hivyo wananchi wakakosa namna nyingine ya kufikisha ujumbe wao kwa serikali, isipokuwa kuandamana.

Hali ikawa mbaya zaidi kiasi cha kuwafanya raia wa Zimbabwe kuukumbuka utawala wa miaka 37 wa aliyekuwa `Rais mbabe kwa nchi za Magharibi', Robert Mugabe aliyeondolewa madarakani kwa nguvu za wanajeshi Novemba 2017.

Raia walioandamana wakaambulia kufyatuliwa risasi zilizosababisha vifo, majeraha, wengine wakikamatwa na kuwekwa ndani huku serikali ikitangaza kuufungia mtandao wa 'intaneti'.

Waziri wa Ulinzi wa Zimbabwe, Owen Ncube, akathibitisha kuhusu kuwapo vifo vya raia vilivyotokea wakati wa maandamano hayo.

Hatua ya vikosi vya ulinzi vya serikali ya Mnangagwa kutumia nguvu kubwa katika kuwadhibiti waandamanaji, inaibua 'kilio cha Wazimbabwe', wakimsihi kiongozi huyo ayaepuke makosa yaliyofanywa na mtangulizi wake, Mugabe.

Maandamano yaliyosababisha vurugu kati ya raia na wanajeshi wa vikosi vya usalama, yakasambaa hususani katika majiji ya Harare na Bulawayo lililo Kusini mwa nchi hiyo.

Baadhi ya Wazimbabwe wakazifunga barabara kuu na kuwalazimisha wafanyakazi wa vituo vya mafuta vilivyokuwa vinatoa huduma hiyo kufunga.

"Tumeteseka vya kutosha," akakaririwa muandamanaji mmoja akisema mjini Bulawayo...hivi sasa serikali inatambua kwamba haturidhishwi na sera zao mbovu kama hii ya kupanda kwa bei ya mafuta."

Chama kikuu cha upinzani nchini humo, Movement for Democratic Change (MDC), kikatoa tamko la kuwataka watu kuwa watulivu .

"Tumekuwa tukiionya serikali hii kuna haja ya kuzungumza...hakuna kilichofanyika. Haya ni matokeo ya unapowakandamiza raia," akasema msemaji wa MDC, Jacob Mafume.

Msemaji wa Serikali, Nick Mangwana, katika taarifa yake akawashutumu waratibu wa maandamano hayo kwa kuwa na ajenda za kisiasa.

Machafuko hayo yaliyoitia doa serikali yakamuibua Rais Mnangagwa ambaye aliahidi kuwa uchunguzi utafanyika kutokana na matumizi makubwa ya nguvu za kijeshi wakati wa maandamano ya kupinga ongezeko maradufu la bei ya mafuta ya petroli na dizeli nchini humo.

Makundi ya haki za binadamu yakabainisha kuwa kiasi cha angalau watu 12 walidaiwa kuuawa na wengine zaidi ya 80 kujeruhiwa katika mashambulizi ya askari wa ulinzi.

Zaidi ya watu 700 walikamatwa, wakiwamo wabunge 11 wa vyama vya upinzani huku taarifa za kidaktari zikielezea kuwapo alama zinazoashiria kupewa `mateso makali'.

Kupanda kwa bei hiyo kulizifanya bidhaa za petroli na dizeli kuwa za ghali zaidi katika ukanda wa bara la Afrika.

Serikali ikamtupia lawama Rais aliyeondolewa madarakani kwa nguvu za jeshi, Mugabe, kwamba utawala wake ulidhorotesha uchumi wa nchi na kusababisha mfumuko wa bei kufikia asilimia 40, hali inayosababisha athari za kiuchumi zikiwemo ukosefu wa ajira na ubovu wa miundombinu.

> Mchungaji Mawarire anasema 'inavunja moyo' kuona serikali ya Rais Mnangagwa inatenda kama ilivyokuwa wakati wa utawala wa Mugabe.

Lakini Rais Mnangagwa anatajwa kuwapo kwenye mfumo wa serikali iliyosababisha madhira hayo akiwa Makamu wa Rais kabla ya kufukuzwa na kukimbilia uhamishoni, Afrika Kusini.

Moja ya sababu zilizotajwa kwa Rais huyo kuziba nafasi ya Mugabe na baadaye kuchaguliwa kupitia sanduku la kura, ilikuwa ni ngome yake katika chama tawala cha Zanu-PF na udhaifu wa mgombea urais kupitia chama cha upinzani cha Movement for Democratic Change (MDC).

Pia palikuwa na hisia kwamba licha ya kuwa mwanasiasa mzee, lakini Rais Mnangagwa alitarajiwa kurejesha hali ya utulivu nchini humo.

Katika moja ya mikutano yake ya kampeni za uchaguzi jijini Harare, binti wa Rais Mnangagwa, Farai Mnangagwa Mlotshwa, alisema, "Baba anajua makosa yalifanyika na kwa namna tofauti, ndiye pekee mwenye uwezo wa kurekebisha na kuyaweka mambo kuwa sawa."

Pia binti huyo akasema baba yake (Mnangagwa) aliwahi kumwambia kwamba ataitumikia nafasi hiyo (Urais) kwa muhula mmoja na kuongeza, "amekuwapo kwa muda mrefu na ana uzoefu unaohitajika."

Lakini wazo kwamba uzoefu wa muda mrefu katika uongozi wa Rais Mnangagwa, ungesaidia kurekebisha makosa yaliyofanyika na kuijenga jamii huru, ilitarajiwa na wengine wengi wakiwamo wana diplomasia wa Magharibi ikiwamo Uingereza.

Lakini hatua zilizochukuliwa na vikosi vya usalama kuwafyatulia risasi raia, kuwapiga, kuwakamata na kufungia mitandao ya kijamii kwa sababu ya kupinga ongezeko la bei ya mafuta haviitofautishi serikali hii na ile ya Mugabe.

Na hii ni kwa mara ya kwanza, kuwapo matumizi makubwa ya nguvu za vikosi vya usalama tangu kuanguka kwa utawala wa Mugabe.

Wakati wa kupinga matokeo ya uchaguzi yaliyozua utata, kulikuwa na taarifa za watu kupigwa risasi wakati vikosi vya majeshi vilipotumia silaha kubwa katikati ya jiji la Harare.

Taarifa zinazohusu kuwapo hali ya kugombania madaraka ndani ya serikali ya Rais Mnangagwa zinaendelea kusambaa, pengine zikihusishwa na machafuko kama maandamano hayo.

Ikiwa Rais Mnangagwa anaweza kuwawajibisha wahusika katika vikosi vya usalama waliowatesa na kuwaua raia, na huenda anataka hivyo, inasubiriwa, lakini matarajio ya kuona haki inatendeka ni madogo sana.

Profesa Patrick Bond wa Chuo Kikuu cha Witwatersrand cha jijini Johannesburg, Afrika Kusini anaviita vitendo vilivyofanywa na vikosi vya usalama nchini Zimbabwe ni vya kutisha dhidi ya raia wa nchi hiyo, kwa vile vimesababisha vifo, majeruhi, watu kukamatwa na kufungwa kwa ajili ya mitandao ya kijamii.

Bond anasema maandamano ya Januari 14-17, mwaka huu yaliitishwa na vyama vya wafanyakazi nchi nzima kupinga ongezeko la mafuta ya petroli na dizeli, hivyo kuirejesha hali kama ilivyokuwa katika utawala wa Mugabe.

Anasema vikosi vya usalama vilienea kwenye miji mingi nchini humo vikihusika kuwapiga hata 'wamachinga' waliokuwa wanajitafutia ridhiki yao mitaani, wakidaiwa kuandamana.

Taasisi ya vyombo vya habari Kusini mwa Afrika (MISA) tawi la Zimbabwe, likatuma ujumbe kupitia kampuni kubwa ya mawasiliano nchini humo ya Econet, kuikosoa serikali ya Rais Mnangagwa kwa kuzuia mtandao wa 'intaneti'.

Mchungaji maarufu aliye pia mwanaharakati, Evan Mawarire, anayeweza kukabiliwa na mashitaka 20 ya mapinduzi kwa kuhamasisha watu kutotii (amri ya serikali) kupitia mtandao wa kijamii, ni miongoni mwa waliokamatwa katika maandamano hayo.

Mchungaji Mawarire anasema 'inavunja moyo' kuona serikali ya Rais Mnangagwa inatenda kama ilivyokuwa wakati wa utawala wa Mugabe.

Kasi ya jumuiya za kimataifa kuvitaka vikosi vya usalama nchini humo kujirekebisha ikaongezeka wakati huo Mnangagwa alikuwa akijiandaa kuwavutia wawekezaji katika Mkutano wa Dunia wa Uchumi uliokuwa unafanyika Davos, Switzerland.

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia namba +255 754 691540.**



## Jeshi la Polisi lashikilia wanne ukwepaji kodi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wanne wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa makosa mbalimbali akiwamo kuingiza uyoga aina ya Soya Gold na mifuko laini ya plastiki kutoka nchini Malawi bila kulipia kodi.

Katika tukio hilo, Musa Maulidi (23), ambaye anatuhumiwa kuingiza bidhaa hizo bila kulipa ushuru.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na paketi 750 na marobota matatu ya karatasi ambavyo vyote havikuwa na nyaraka zinazoonyesha kuwa amelipa kodi.

Alisema alikamatwa katika eneo la kizuizi cha barabara kilichoko eneo la Kayuki barabara kuu ya Tanzania na Malawi wilayani humo, majira ya saa 12 :45 asubuhi akisafirisha bidhaa hizo kutoka Kyela kuelekea Mbeya.

"Mtuhumiwa kwa sasa yupo mahabusu na tunakusudia kumpeleka mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria, ili kukomesha vitendo hivi ambavyo vimekithiri katika barabara hiyo," alisema Kamanda Matei.

Katika tukio la pili Kamanda Matei alisema kijana mmoja ajulikanaye kwa jina la Bahati Kasungula (35), alikamatwa akisafirisha vitenge kutoka nchini Malawi kuingiza katika Mkoa wa Mbeya.

Alisema mtuhumiwa huyo pia alikamatwa katika kizuizi cha barabara cha Kayuki ambacho kimekuwa maarufu kwa kukamata wakwepa kodi wanaoingiza bidhaa kutoka nchini Malawi kwa kupitia njia za panya na hivyo kukwepa kodi.

Katika tukio la tatu Kamanda Matei alisema kijana mwingine, Juhudi Kasyupa (25), mkazi wa Majengo katika Wilaya ya Chunya, alikamatwa na jeshi hilo akiwa anamiliki mali mbalimbali za wizi.

Alizitaja baadhi ya mali ambazo kijana huyo alinaswa nazo kuwa ni pamoja na boksi moja la daftari, deki, kompyuta, betri za solar, runinga, kopo la rangi na solar panel.

Alisema baada ya mtuhumiwa kupekuliwa alikutwa na vifaa mbalimbali vya kuvunjia nyumba zikiwamo nondo, bisi bisi na kwamba vitu hivyo vilikutwa nyumbani kwa mtuhumiwa na kwamba alipohojiwa hakuwa na maelezo ya kujitosheleza.

Katika tukio la mwisho, Kamanda Matei alimtaja kijana mwingine kuwa ni Juma Adamu (23) mkazi wa Mbozi mkoani Songwe ambaye alikutwa na mali za wizi.

# Waziri Lukuvi aponda Jiji la Mbeya kwa ujenzi holela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema Jiji la Mbeya ndiyo mji unaoongoza nchini kwa mpangilio mbovu wa makazi ya wananchi kutokana na maofisa mipango miji wake kutotekeleza majukumu yao ipasavyo.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na watumishi wa Idara ya Ardhi wa Halmashauri za Wilaya ya Mbeya pamoja na ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini baada ya kufanya ziara ya kushtukiza kwenye ofisi ya Jiji la Mbeya. Alisema kuwa sehemu kubwa ya makazi ya wananchi yamejengwa kiholela kutokana na kutokuwapo kwa mpangilio ulioandaliwa na wataalamu wa mipango miji wa jiji hilo pamoja na wapima ardhi.

"Mbeya ni Jiji lakini ni miongoni mwa miji inayonikera sana, halina 'master plan' wananchi wanajipanga wenyewe kulingana na kila mtu anaponunua eneo, sasa naendelea kufuatilia na kama hali itaendelea kuwa hivi itabidi niwahamishie kwenye halmashauri zingine," alisema Lukuvi.

**Kuanzia mwezi Machi mwaka huu, serikali inakusudia kuanza kutoa leseni za makazi kwa wananchi wanaomiliki nyumba nchini ili kila nyumba iwe inalipiwa.**

Waziri Lukuvi alisema jiji hilo lina malimbikizo ya kodi za pango la ardhi kutokana na maofisa wanaohusika kutokusanya fedha hizo kwa wananchi wanaostahili kulipia kodi licha ya kupewa malengo na wizara yake.

Aidha, alisema kuanzia mwezi Machi mwaka huu, serikali inakusudia kuanza kutoa leseni za makazi kwa wananchi wanaomiliki nyumba nchini ili kila nyumba iwe inalipiwa.

Alisema leseni hizo zitakuwa zinadumu kwa miaka mitano ili baada ya hapo mmiliki awe tayari amehama na kuwa na hati miliki ya nyumba yake badala ya kuendelea kuitumia.

Waziri Lukuvi alifafanua kuwa leseni hizo zitakuwa zinaonyesha ukubwa wa eneo analomiliki mwananchi, aina ya nyumba aliyojenga na kiwango cha kodi ya serikali anayostahili kulipa na kwamba wananchi watakuwa na uwezo wa kuzitumia leseni hizo kukopa fedha kwenye benki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, James Kasusura, alikiri eneo lake kujengwa holela na kwamba asilimia zaidi ya 90 ya makazi hayajapangwa.

Alisema kuwa kwa sasa Jiji hilo linakusudia kupima zaidi ya viwanja 50,000 kwa ajili ya mji mpya utakaojulikana kwa jina la New Mbeya City katika eneo la Nsoho.

Alisema upimaji wa mji huo pamoja na uandaaji wa michoro unafadhiliwa na Benki ya Dunia na kwamba tayari wameshaanza kufanya taratibu za kuanza kulipima.

"Mpaka sasa nimemtuma ofisa ardhi jijini Dodoma kwa ajili ya kufuatilia, amesafiri usiku kucha na ameniambia amefika alfajili ya leo (juzi) tayari kwa kwenda kufuatilia taratibu na hawa wenzetu kwa ajili ya kupima," alisema Kasusura.

Awali waziri Lukuvi aliwahoji maswali mbalimbali maofisa ardhi na maofisa mipango miji kuhusu utendaji wao wa kazi, ambapo alisema alikuwa anauliza maswali hayo kwa ajili ya kuwapima kama wana mipango kazi waliyojiwekea.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yusuf Masauni, akiweka mchanga juzi, katika moja ya makaburi ya watoto watatu wa familia moja waliouawa kikatili katika kijiji cha Ikando Kata ya Kichiwa, wilayani Njombe. **PICHA: WMN**

# Halmashauri yatoa saruji, mabati kuunga mkono wananchi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, imetoa mifuko 600 ya saruji na mabati 300 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 15 vya shule za sekondari za kata ili kuwezesha zaidi ya wanafunzi 636 wa kidato cha kwanza kuanza masomo.

Aidha, halmashauri hiyo imetoa Sh. milioni 15 kwa ajili ya kusaidia shughuli za ufundi wakati wa kukamilisha vyumba hivyo ambavyo vimejengwa kwa nguvu za wananchi.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Hunter Mwakifuna, alisema mbali na michango hiyo pia Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameichangia wilaya hiyo mabati 360.

Mwakifuna alisema upungufu wa vyumba hivyo vya madarasa umesababishwa na ufaulu mkubwa wa wanafunzi mwaka huu.

"Fedha hizi tulizochangia zinatokana na makusanyo ya ndani ya halmashauri yanayotokana na ushuru wa mazao mbalimbali, lakini pia tunamshukuru Mkuu wetu wa Mkoa amekuwa mtu wa pekee maana wengine huwa wanaishia kutoa matamko," alisema Mwakifuna.

Aliwapongeza wananchi wa kata za wilaya hiyo kwa michango yao ya hali na mali katika kuhakikisha vyumba vya madarasa vya ajili ya watoto wetu vinajengwa haraka.

Alisema baadhi ya vyumba vya madarasa hayo vimefikia hatua ya kuezeka na mengine tayari yameezekwa na kinachoendelea kwa sasa ni kuweka mbao za kufundishia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Lucy Mganga, alisema anaamini vyumba vyote vitakuwa vimekamilika kufikia Februari 14, ili wanafunzi waliokuwa hawajaanza masomo waanze mara moja ili wasiwe nyuma ya muhula. Alisema yeye kwa kushirikiana na watendaji wake wengine wanashirikiana kila siku kuhakikisha vyumba hivyo vinakamilika ili wanafunzi hao waanze hata kama vitakuwa havijakamilika vizuri.

Aliitaka wilaya hiyo kuendelea kuiunga mkono serikali ya awamu ya tano kwenye miradi mbalimbali akidai kuwa kwa sasa sera ya elimu bure inasaidia kuwapunguzia wananchi michango.

Naye Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Kyela, Prochesius Mguli, aliupongeza uongozi wa halmashauri kwa harakati za kuboresha miundombinu ya shule kwenye wilaya hiyo.





# Jafo atoa wiki 3 mhandisi kumaliza kituo cha afya

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ametoa wiki tatu kwa mhandisi anayesimamia kituo cha afya cha Mkonze jijini Dodoma, Francis Bago, kukamilisha ujenzi.

Waziri Jafo alitoa kauli hiyo wakati alipokuwa akikagua miradi mikubwa inayotekelezwa na serikali ndani ya Jiji la Dodoma.

Jafo alisema kuwa ndani ya wiki tatu ujenzi wa kituo hicho uwe umekamilika kwa kuwa uko nyuma ya wakati ukilinganisha na maeneo mengine.

Alisema ni uzembe kuona kituo hicho hakijakamilika wakati vituo vilivyopo vijijini ujenzi wake umekamilika na mgao wa fedha ulitoka kwa wakati mmoja.

**Naagiza pia kituo hiki kuhakikisha kuwa kinajengwa kwa viwango vinavyotakiwa ili kuepuka kutitia pindi kikianza kutumika.**

"Nashangaa kuona kituo hiki kipo mjini kabisa ujenzi wake haujakamilika, wakati huo huo kuna vituo vimekamilika na vipo mbali na vifaa vya ujenzi vinapatikana kwa umbali mrefu, kwa hiyo huu ni uzembe na naagiza ndani ya wiki tatu ujenzi huu uwe umekamilika," alisema.

Serikali ilitoa kiasi cha Sh. milioni 400, kukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya, kiasi ambacho kilipelekwa katika halmashauri nyingi ili kuhakikisha vituo vya afya vinajengwa.

Vile vile amemtaka mhandisi mshauri wa Jiji la Dodoma kuhakikisha mradi wa ujenzi wa kituo cha kuegesha magari makubwa kilichopo Nala kukamilika kwa wakati ili kuanza kutumika.

"Naagiza pia kituo hiki kuhakikisha kuwa kinajengwa kwa viwango vinavyotakiwa ili kuepuka kutitia pindi kikianza kutumika," alisema.

Jafo alisema ameridhishwa na hatua ya ujenzi wa miradi miwili ya stendi kubwa ya mabasi na soko kubwa linalojengwa eneo la Nanenane na kampuni ya Mohamed Bulder, na kusisitiza usimamizi thabiti ili miradi hiyo iwe kioo ndani ya Jiji la Dodoma.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kuanza mapema kupanga namna ya uendeshaji wa miradi hiyo ili iweze kuleta tija kwa serikali na kuwa chachu ya maendeleo ndani ya jiji hilo.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Maimuna Tarishi, akiteta jambo na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Alvaro Rodriques, wakati wa warsha ya kupunguza madhara ya maafa nchini na kuimarisha uthabiti kwa nchi na jamii dhidi ya majanga ya asili katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, jijini Dodoma juzi. **PICHA: OWM**

# Watu 71 wapoteza maisha kwa mafuriko, 64 majeruhi mwaka 2018

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

WATU 71 wamepoteza maisha na wengine 64 kujeruhiwa kwa mwaka jana kati ya mwezi Januari hadi Desemba 2018 kutokana na mafuriko yaliyotokea hapa nchini.

Aidha, nyumba 15,802 zimeharibiwa kwa viwango tofauti, kuathiri miundombinu katika shule 43, mashamba ya mazao na vituo vya afya.

Akitoa takwimu hizo jana wakati akifungua warsha ya kupunguza madhara ya maafa nchini, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Maimuna Tarishi, alisema miaka ya hivi karibuni maeneo mbalimbali ya nchi yamekuwa yakikumbwa na ukame wa mara kwa mara.

"Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, tangu tupate uhuru nchi imeathiriwa na ukame kwa zaidi ya mara 18 ambapo matukio makubwa ya ukame ni pamoja na yale ya mwaka 2006/2007 na 2007/2008 ambayo yaliathiri zaidi mikoa ya Arusha na Dodoma," alisema Maimuna.

Alisema mikoa mingine iliyoathiriwa ni pamoja na Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Shinyanga, Lindi, Singida, Tabora na Mwanza.

Alisema kuwa ukame mwingine mkubwa ulitokea mwaka 2008/2009 ulioathiri zaidi mikoa ya kaskazini ya nchi hasa Arusha na Manyara.

"Mikoa ambayo mara nyingi huathiriwa na ukame ni Dodoma, Singida, Tabora na Shinyanga, ambayo kawaida hupata mvua ya chini kwa kiwango cha kati ya milimita 200 - 600 kwa mwaka," alisema Maimuna.

Alisema mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano, 2016/17-2020/21 unaelezea umuhimu wa kuimarisha ustahimilivu wa majanga ya asili kwa njia ya mikakati mbalimbali.

# Waitara atoa maagizo mazito ujenzi wa shule

**Na Ibrahim Joseph**, DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mwita Waitara, amewaagiza wakurugenzi na maofisa elimu kuhakikisha kuwa wanasimamia na kufuatilia miradi ya ujenzi wa miundombinu ya shule.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akifungua mafunzo elekezi kuhusu utekelezaji wa programu ya lipa kulingana na matokeo katika sekta ya elimu (EPror R) yaliyofanyika jijini hapa.

Waitara aliwaagiza Wakurugenzi wote pamoja na halmashauri na maofisa elimu kusimamia na kufuatilia miradi ya ujenzi ya miundombinu ya shule inayoendelea kote nchini.

Alisema pamoja na kusimamia wanatakiwa kuhakikisha inakamilika kwa wakati na pasiwepo na visingizio vya kuchelewesha.

Pia aliwataka kuhakikisha ujenzi wa miradi hiyo ya shule inaendana na thamani halisi ya fedha zilizotolewa na serikali pamoja na wahisani.

Alisema ujenzi wa majengo mbalimbali uzingatie ramani zitakazotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Aidha, alisema kuwa fedha zitakazotolewa kwa ajili ya motisha zaidi ya zile zilizo kwenye maelekezo hazitakubaliwa mpaka pale halmashauri zitakapoomba kibali cha kubadili matumizi.

Alibainisha kuwa fedha zinazopelekwa kwenye elimu kwa ajili ya matumizi mbalimbali zitumike kama ilivyokusudiwa.

"Naomba nichukue fursa hii kuwakumbusha na kuwasisitiza kuwa matumizi mengine yoyote ya fedha za motisha zaidi ya yale mtakayoelekezwa hayatakubalika mpaka pale halmashauri zitakapoomba kibali cha kubadili matumizi nje ya maelekezo yaliyotolewa na kuruhusiwa," alisema Waitara.

Aliwataka wasifumbie macho kesi za wanaowapa mimba mwanafunzi kwa kuwa wamekuwa wakikatisha ndogo za wasichana hao wakati wahusika wakiendelea kufanya vitendo hivyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu wa Elimu Ofisi ya Rais Tamisemi, Julius Nestory, alisema programu ya lipa kulingana na matokeo katika sekta ya elimu ilizinduliwa Septemba 2014 chini ya mpango wa matokeo makubwa sasa kwa lengo la kuinua ubora wa elimu nchini.

Nestory alisema kupitia programu hiyo fedha hutolewa kwa kukidhi vigezo vilivyokubalika baada ya kufanyiwa uhakiki na kuthibitika mfumo unaosaidia kuhakikisha kuwa vipaumbele vya sekta ya elimu vinatekelezwa kwa kuzingatia mipango ya bajeti iliyoidhinishwa na bunge kwa mwaka husika.

Alisema utekelezaji wa programu hiyo umeleta faida nyingi ikiwamo utamaduni wa kutumia rasilimali zilizopo kwa ufanisi katika utekelezaji malengo waliyojiwekea ili kuleta maendeleo endelevu.

Pia kuchochea ushiriki wa jamii katika masuala ya kielimu ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya shule

Aidha, kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa rasilimali fedha na manunuzi ya umma kwa ajili ya mipango ya elimu.



# Z'bar yaahidiwa neema sekta mbalimbali kukuza uchumi

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

BALOZI wa Kuwait nchini, Mubarak Mohammed Al - Sehaijan, amesema nchi yake itaendelea kutoa msaada katika sekta mbalimbali ili kuhakikisha mafanikio ya kiuchumi yanapatikana.

Kuwait imekuwa ikitoa misaada katika sekta za kiuchumi na maendeleo Zanzibar ikiwamo kwenye afya, elimu na mawasiliano kupitia Kuwait Fund.

Balozi huyo alisema Zanzibar ina nafasi ya kutumia fursa iliyotolewa na nchi yake, kuainisha maeneo ambayo inahitaji kusaidiwa ili kuimarisha na kukuza miradi ya wananchi.

Mwanadiplomasia huyo aliyasema hayo wakati akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alipofika ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar kujitambulisha rasmi.

**Zanzibar ina historia za kibiashara kati yake na mataifa yaliyopo Ghuba ya Uajemi, ambayo inapaswa kujumuishwa katika ajenda hiyo itakayosaidia kuieneza kwa kizazi cha sasa na kijacho.**

"Zanzibar inapaswa kutafakari maeneo mapya ya kuungwa mkono, Kuwait imeshaandaa mpango maalum wa kukisaidia Chuo Kikuu cha Sumeit kilichoko Chukwani nje kidogo ya Mji wa Zanzibar kwa kukiongezea nguvu kwenye fani za Biashara na Sayansi," alisema Mubarak.

Balozi Mubarak alisema hatua hiyo imelenga kustawisha jamii ya Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla katika masuala ya taaluma, ambayo ni muhimu katika mazingira ya binadamu, hasa ikizingatiwa mabadiliko makubwa ya kasi ya sayansi na teknolojia yanayoizunguka dunia kwa sasa.

Kuhusu sekta ya utalii inayozidi kushika kasi Zanzibar, Balozi huyo alisema wakati umefika kwa taasisi zinazosimamia sekta hiyo kuwa na ajenda maalum ya kuyatangaza maeneo yenye vivutio vya utalii.

Alisema Zanzibar ina historia za kibiashara kati yake na mataifa yaliyopo Ghuba ya Uajemi, ambayo inapaswa kujumuishwa katika ajenda hiyo itakayosaidia kuieneza kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Kwa upande wake Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema uimarikaji wa sekta ya afya kwa kuongezeka vifaa vya kisasa pamoja na miundombinu ya mawasiliano ya barabara inayotokana na misaada ya nchi hiyo kumeleta faraja kwa wananchi wanaoendelea kupata huduma kupitia miradi hiyo.



Wafanyabiashara mkoani Shinyanga wakipewa elimu ya kusajili biashara zao Brela kwa kutumia mfumo mpya wa mtandao. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Serikali yakubali jukumu la kutoa ajira kwa vijana

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema serikali inalo jukumu la kutoa ajira kwa wanafunzi waliohitimu masomo yao nchini Oman ili watumie vizuri ujuzi walioupata.

Akizungumza na wanafunzi saba waliorejea nchini, alisema serikali inataka kuona ni kwa kiasi gani inawasaidia ili kuhakikisha wanapata ajira katika sekta za umma au binafsi endapo watawahitaji.

Pembe alisema kuna baadhi ya watu wanaweza kuwashawishi vibaya na kusababisha wapoteze mwelekeo katika maisha yao na kwamba wawe makini na hilo wakati huu ambao serikali inashughulikia ajira zao.

Alisema fani walizozichagua ni muhimu na ndiyo vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa vile inahitaji wahandisi katika maeneo mbalimbali ikiwamo uchoraji wa ramani, ujenzi wa nyumba, barabara, mafuta na gesi na viwanda mbalimbali.

"Kitendo chenu cha kupokea nafasi hizo za masomo za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kukubali kujiunga na vyuo vya Oman kimeleta heshima nzuri pamoja na kuitangaza vizuri Zanzibar na itasaidia kupata nafasi nyingine zaidi, ambazo hutolewa kila mwaka nchini humo," alisema Pembe.

Naye Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo Zanzibar, Iddi Khakis, alisema hadi sasa kuna wanafunzi 21, waliokwenda nje ya nchi, kati yao watano wamepata ufadhili wa kulipiwa na wengine wana ufadhili nusu, lakini jitihada za serikali ni kuendelea kuhakikisha waliobaki wanapata ufadhili uliobakia.

Kwa upande wa wanafunzi hao wamempongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa juhudi alizozichukua kuhakikisha wanapata nafasi za masomo nje ya nchi na wameahidi kuwa wazalendo kwa ajili ya kuitumikia nchi yao.

# Vijana watakiwa kuchangamkia fursa

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

VIJANA nchini wametakiwa kutumia fursa mbalimbali za ujasiriamali zilizopo kuongeza taaluma ili waweze kunufaika wao na jamii kwa ujumla.

Akifunga mafunzo ya siku mbili kwa wajasiriamali kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, Mkuu wa Wilaya ya Magharibi A, Kapten Khatib Khamis Mwadini, alisema serikali imekuwa ikiwekeza katika taaluma mbalimbali ili kuongeza fursa za kujiajiri.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya aliwataka vijana kujikusanya na kuunda ushirika ili kufikia fursa mbalimbali zilioko ikiwa ni pamoja na kupatiwa mtaji sambamba na masoko kwa shughuli wanazozifanya.

Mwadini pia alipata fursa kuangalia kazi mbalimbali za mikono zilizofanywa na baadhi ya wajasiriamali hao.

Kwa upande wa wajasiriamali waliopata mafunzo hayo walisema elimu hiyo itawajengea uwezo na kuongeza uelewa kwa kazi wanazozifanya na kufanya shughuli zao kwa tija.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Khadija Sadik, aliziomba taasisi za serikali zinazohusika na uwezeshaji wa vijana kubaini changamoto zinazowakabili wajasiriamali na kuzipatia ufumbuzi wa kitaalamu.

Mafunzo hayo ya siku mbili yalitolewa na taasisi mbili za NECOC kutoka Zanzibar na TAEDO ya Tanzania Bara, ambapo wajasiriamali walifundishwa ufugaji, ukulima na utengenezaji wa bidhaa.

ITV
Daima
Kwa matangazo na Burudani saa 24

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 28 Jan**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt :
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 29 Jan**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 30 Jan**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 31**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 01 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 2 Feb**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Fangs
23:00 The other side rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 03 Jan**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice Inkulo
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima — WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 28 Jan**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Shamba shape up
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 29 Jan**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Documentary: Living on the edge
21:30 Kipindi maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 30 Jan**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Biko Draw
21:05 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kipindi Maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 31 Jan**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Hatua
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Living on the edge rpt
13:30 Jungu Kuu
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Huduma ya kwanza rpt
18:30 Kipindi Maalum: Ewura
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 01 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi maalum: Tanesco
13:30 Kipindi Maalum rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Mapishi
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Uchumi na biashara
19:00 Kipindi maalum: TCRA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 02 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Hatua
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 03 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Fundi Rama
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:00 Biko draw
21:05 Mizengwe
21:30 3Mzuka
22:00 Bongo Movie: Fundi Rama 2
23:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


EATV

LEO ASUBUHI SAA 5:00

DADAZ

JUMATANO
10:59 Jikoni Na Jane
11:00 DADAZ (live)
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
20:00 EPL REVIEW
21:00 Supa Mzuka Jackpot
21:30 Mid Week Movie




**DADAZ** Kipindi kinachompatia mwanamke nafasi ya kuzungumza maswala ya kijamii, afya, siasa na uchumi ambayo yanayoizunguka jamii

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One — WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| - Hasara Katika Mali | -495 | 738 | 243 | 4,123 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 101 | 218 | 319 | -265 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 1 | (1) | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 12,901 | -10,647 | 2,254 | 4,906 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | 1,875 | 1,226 | 3,101 | -5,635 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 53 | -319 | -266 | 855 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,359 | 503 | 1,862 | -353 |
| - Kodi Iliyolipwa | (9) | 9 | - | - |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | (41) |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **15,374** | **(9,426)** | **4,678** | **(2,794)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - | - | (23) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | 369 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | - | - | - | 346 |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | 2,581 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (2,242) | - | (2,242) | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(2,242)** | **-** | **(2,242)** | **2,581** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 13,132 | (9,426) | 2,436 | 133 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 7,691 | 9,582 | 7,691 | 21,268 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **10,127** | **7,691** | **10,127** | **21,401** |

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| XIONG ZHENGLIN (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ...................... | **1/29/19** |
| HENRY B. KYOMBO (Mkuu wa Fedha) | ...................... | **29/Jan/19** |
| VICTORIA EDWARD (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ...................... | **29/Jan/19** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **LIU LIN**<br>**MJUMBE WA BODI** | ...................... | **29/Jan/19** |
| **JIANG CHAO**<br>**MJUMBE WA BODI** | ...................... | **29/Jan/19** |

## The Banking and Financial Institutions (Disclosures) Regulations, 2014
## MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES
## (Made under Regulation 11)

| No. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | **TZS** | | **USD** | |
| | (a) Required minimum opening balance | | | | |
| | Personal Current Account | TZS | 100,000.00 | $ | 100.00 |
| | Business Account | TZS | 200,000.00 | $ | 200.00 |
| | Imperial Business Account | TZS | 5,000,000.00 | $ | 5,000.00 |
| | Community Account | TZS | 200,000.00 | $ | 200.00 |
| | Call Account | TZS | 10,000,000.00 | $ | 10,000.00 |
| | (b) Monthly service fee (break down per customer type) | | | | |
| | Personal Current Account | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Business Account | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Imperial Business Account | TZS | 25,960.00 | $ | 25.96 |
| | Community Account | Free | | Free | |
| | Call Account | Free | | Free | |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS | 1,947.00 | 0.75% of withdrawal amount | |
| | (d) Fees per ATM Withdrawal | | | | |
| | Personal Savings (5 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Imperial Savings (5 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Student Boom Account | TZS | - | $ | - |
| | Junior Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | Senior Savings Account (3 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Personal Current Account | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | (e) ATM mini statement | TZS | 300.00 | $ | - |
| | (f) Interim statement (Below 3 months) | TZS | 3,894.00 | $ | 2.60 |
| | (g) Periodic scheduled statement | Free | | Free | |
| | (h) Cheque book (per leaf) | TZS | 519.20 | $ | 0.52 |
| | (i) Dishonoured Cheque | | | | |
| | Inward Unpaid Cheque | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Outward Unpaid Cheque | TZS | 38,940.00 | $ | 38.94 |
| | (j) Special clearance | | | | |
| | Personal Accounts | TZS | 51,920.00 | $ | 51.92 |
| | Business Accounts | TZS | 64,900.00 | $ | 64.90 |
| | (k) Counter cheque (per leaf) | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (l) Stop payment (per leaf) | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (m) Standing order | | | | |
| | Internal | Free | | Free | |
| | External | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Unpaid | TZS | 6,490.00 | $ | 6.49 |
| | (n) Balance enquiry | Free | | Free | |
| | (o) New ATM card issuance | Free | | Free | |
| | (p) ATM card renewal or replacement | TZS | 12,980.00 | $ | - |
| | (q) Overdrawn Account interest charge | 10% above the Banks Base Lending Rate | | | |
| | (r) Unarranged overdraft | 10% above the Banks Base Lending Rate | | | |
| | (s) Interbank transfer | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (t) Bill payments through ATM | TZS | 713.90 | $ | - |
| | (u) Deposit fee | Free | | Free | |
| | (v) Other (please specify) | | | | |
| | ATM withdrawal limit per transaction | TZS | 400,000.00 | $ | - |
| | ATM withdrawal daily limit | TZS | 1,000,000.00 | $ | - |
| 2 | **Savings Accounts** | | | | |
| | (a) Required minimum opening balance | | | | |
| | Personal Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Student Boom | TZS | 20,000.00 | $ | 20.00 |
| | Senior Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Joint Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Imperial Savings Account | TZS | 2,000,000.00 | $ | 2,000.00 |
| | Junior Savings Account | TZS | 10,000.00 | $ | 10.00 |
| | (b) Monthly service fee | | | | |
| | Personal Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9.09 |
| | Student Boom | Free | | Free | |
| | Senior Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9,086.00 |
| | Joint Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9,086.00 |
| | Imperial Savings Account | TZS | 19,470.00 | $ | 19.47 |
| | - Imperial Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | - Imperial Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | - Junior Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | (e) Deposit rate (Personal savings accounts) | | 2.5% | $ | 0.01 |
| 3 | **Electronic Banking** | | Free | | Free |
| | (a) Internet Banking monthly fee | | FREE | | FREE |
| | (b) Internet transfers | | FREE | | FREE |
| | (c )SMS Banking | | NA | | NA |
| | (d) Other | | | | |
| | E-Banking Statement request(Self downloaded) | | FREE | | FREE |
| | E-Banking Password resetting | | FREE | | FREE |
| | E-Banking Statement request (printed by the Bank) per page | | TZS 1,298 | | $1.298 |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | | | | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the counter | | - | | - |
| | (b) Purchase of foreign cheque | | - | | - |
| | (c) Sale/Purchase of cash passport | | - | | - |
| | (d) Telegraphic Transfer (TISS/RTGS) | | | | |
| | Outward TT | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Inward TT | | Free | | Free |
| | (e) Telex/Swift | | | | |
| | Outward TT | | | $ | 64.90 |
| | Inward TT | | | $ | 12.98 |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated Account to local current Account ( within bank and to other bank) | | - | | - |
| 5 | **Loans** | | | | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | | | |
| | (i) Personal loans | 2% of the facility amount | | | |
| | (ii) Overdrafts | 2% of the facility amount | | | |
| | (iii) Mortgage finance | 2% of the facility amount | | | |
| | (iv) Asset finance | 2% of the facility amount | | | |
| | (b) Unpaid loan instalment | 10% above interest rate | | | |
| | (c) Early repayment | 3% of amount to be settled early | | | |
| | (d) Valuation fees | As per service provider rates | | | |
| | (e) Legal Fees | As per service provider rates | | | |
| | (f) Base Lending Rates | | 21% | $ | 0.09 |
| | (g) Maximum Spread Above the Base Lending Rate (BLR) | | 5% | $ | 0.05 |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Signature | Designation | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Xiong Zhenglin | | Chief Executive Officer | 29.01.2018 |
| 2 | Joseph Phales | | Ag: Head of Business & Operations | 29.01.2018 |

**TANGAZO**

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED

## ISSUED PURSUANT TO REGULATIONS 7 AND 8 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2014

### CONDENSED STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT THE QUARTER ENDED 31/12/2018

(Amounts in shillings)

| | | Crrent Quarter Date: 31.12.2018 | Previous Quarter Date: 30.09.2018 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **ASSETS** | | |
| 1 | Cash | 8,057,402 | 9,001,072 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | 431,181,636 | 378,982,162 |
| 3 | Investments in Government securities | - | - |
| 4 | Balances with other banks and financial institutions | 1,979,765,030 | 1,575,655,326 |
| 5 | Cheques and items for clearing | 1,023,222,118 | - |
| 6 | Inter branch float iterms | - | - |
| 7 | Bills negotiated | - | - |
| 8 | Customers' liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans Receivables | - | - |
| 10 | Investments in other securities | - | - |
| 11 | Loans, advances and overdrafts (net of allowances for probabl | 377,305,551 | 1,563,022,842 |
| 12 | Other assets | 2,071,834,371 | 2,416,612,404 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwriting accounts | - | - |
| 15 | Property, Plant and Equipment | 1,229,186,706 | 1,245,058,938 |
| **16** | **TOTAL ASSETS** | **7,120,552,814** | **7,188,332,744** |
| **B.** | **LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and financial institutions | - | - |
| 18 | Customer deposits | 5,139,155,552 | 5,427,732,635 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special deposits | - | - |
| 21 | Payment orders/transfers payable | - | - |
| 22 | Bankers' cheques and drafts issued | 452,122,099 | (636,603,701) |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | 19,060,491 | 88,095,756 |
| 24 | Acceptances outstanding | - | - |
| 25 | Interbranch float items | - | - |
| 26 | Unearned income and other deferred charges | - | - |
| 27 | Other liabilities | 180,479,418 | 48,141,461 |
| 28 | Borrowings | - | - |
| 29 | **TOTAL LIABILITIES** | **5,790,817,560** | **4,927,366,151** |
| 30 | **NET ASSETS/(LIABILITIES)(16 minus 29)** | **1,329,735,254** | **2,260,966,593** |
| **C.** | **SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 7,363,802,064 | 6,897,692,064 |
| 32 | Capital reserves | 453,542,327 | 453,542,327 |
| 33 | Retained earnings | (3,873,755,355) | (3,822,156,408) |
| 34 | Profit (Loss) account | (2,623,756,656) | (1,278,689,020) |
| 35 | Other capital accounts | 9,902,874 | 10,577,630 |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| 37 | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **1,329,735,254** | **2,260,966,593** |
| 38 | Contingent liabilities | - | - |
| 39 | Non performing loans & advances | 1,615,762,758 | 1,088,648,034 |
| 40 | Allowances for probable losses | 1,272,968,059 | 424,817,610 |
| 41 | Other non performing assets | 66,083,844 | 43,217,532 |
| **D.** | **SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders Funds to total assets | 18.67% | 31.45% |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 94.14% | 53.60% |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | 33.40% | 37.42% |
| (iv) | Loans and advances to total assets | 5.30% | 21.74% |
| (v) | Earning assets to Total Assets | 4.50% | 20.53% |
| (vi) | Deposits Growth | -5.32% | -4.00% |
| (vii) | Assets growth | -0.94% | -1.71% |

### CONDENSED STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE QUARTER ENDED 31/12/2018

(Amounts in shillings)

| | | Current Quarter Date: 31.12.2018 | Comparative Quarter (Previous Year) Date:31.12.2017 | Current Year Cumulative Date: 31.12.2018 | Comparative Year (Previous Year) Cumulative Date:31.12.2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Interest Income | 39,915,028 | 125,960,443 | 295,320,814 | 492,097,177 |
| 2 | Interest Expense | 25,355,562 | 134,607,502 | 243,211,557 | 437,488,515 |
| 3 | Net Interest Income ( 1 minus 2) | **14,559,466** | **(8,647,059)** | **52,109,257** | **54,608,662** |
| 4 | Bad Debts Written -Off | - | - | - | - |
| 5 | Impairment Losses on :Loans and Advances | 877,730,392 | 36,532,318 | 1,198,259,690 | 39,579,658 |
| **6** | **Non Interest Income:** | **14,043,561** | **518,272,588** | **78,743,507** | **1,671,366,867** |
| | 6.1 Foreign Currency Dealings and Translation Gains/ (Loss) | - | - | - | - |
| | 6.2 Fees and Commissions | 11,389,083 | 30,393,398 | 60,131,480 | 100,358,650 |
| | 6.3 Dividend Income | - | - | - | - |
| | 6.4 Other Operating Income | 2,654,478 | 487,879,190 | 18,612,027 | 1,571,008,217 |
| **7** | **Non Interest Expenses:** | **495,940,270** | **498,378,365** | **1,556,349,730** | **1,656,582,910** |
| | 7.1 Salaries and Benefits | 137,416,106 | 111,015,073 | 590,830,617 | 478,832,702 |
| | 7.2 Fees and Commission | 13,139,914 | 17,903,220 | 58,754,715 | 69,109,724 |
| | 7.3 Other Operating Expenses | 345,384,250 | 369,460,072 | 906,764,398 | 1,108,640,484 |
| **8** | **Operating Income/ (Loss)** | **(1,345,067,635)** | **(25,285,154)** | **(2,623,756,656)** | **29,812,961** |
| **9** | **Income Tax Provision** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **10** | **Net Income / (Loss) After Income Tax** | **(1,345,067,635)** | **(25,285,154)** | **(2,623,756,656)** | **29,812,961** |
| **11** | **Other Comprehensive Income (itemize)** | | | | |
| **12** | **Total Comprehensive Income/(loss) for the year** | **(1,345,067,635)** | **(25,285,154)** | **(2,623,756,656)** | **29,812,961** |
| 13 | Number of Employees | 32 | 33 | 32 | 32 |
| 14 | Basic Earnings Per Share | -97.50 | -83.85 | -190.19 | 98.87 |
| **15** | **Number of Branches** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **SELECTED PERFORMANCE INDICATORS** | | | | |
| (i) | Return on Average Total Assets | -56.67% | -0.88% | -331.63% | 3.13% |
| (ii) | Return on Average Shareholders' Fund | -54.80% | -5.02% | -1775.83% | -15.18% |
| (iii) | Non Interest Expense to Gross Income | 919.11% | 77.36% | 416.06% | 76.57% |
| (iv) | Net Interest Income to Average Earning Assets | -356.49% | -0.74% | -695.393% | 0.87% |

Average figures shall be computed by summing up the end balances for respective months in the period divided by number of months in the period.

### CONDENSED STATEMENT OF CASH FLOW STATEMENT FOR THE QUARTER ENDED 31/12/2018

(Amounts in shillings)

| | | Current Quarter Date:31.12.2018 | Previous Quarter Date:30.09.2018 |
|---|---|---|---|
| I: | **Cash flow from operating activities:** | | |
| | Net income/ (Loss) | (1,345,067,635) | (577,833,909) |
| | **Adjustments for:** | - | - |
| | - Impairment/Amortization | - | - |
| | - Depreciation | 15,872,232 | 15,872,232 |
| | - Net change in Loans and Advances | 1,185,717,291 | 411,201,756 |
| | - (Gain)/loss on Sale of Assets | - | - |
| | - Net change in Deposits | (288,577,083) | (226,039,456) |
| | - Net change in Short Term Negotiable Securities | - | - |
| | - Net change in Other Liabilities | 132,337,957 | (5,822,803) |
| | - Net change in Other Assets | 344,778,033 | 91,873,781 |
| | - Tax Paid | - | - |
| | - Others ( specify) | 383,757,665 | (1,137,022,009) |
| | - Minority interest | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by operating activities*** | **428,818,460** | **(1,427,770,408)** |
| II: | **Cash flow from investing activities:** | | |
| | Dividend Received | - | - |
| | Purcharse of Fixed Assets | - | - |
| | Proceeds from Sale of Fixed Assets | - | - |
| | Purchase of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Proceeds from Sale of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Others (specify) | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by investing activities*** | - | - |
| III: | **Cash flow from financing activities:** | | |
| | Repayment of Long-term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Long Term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | 466,110,000 | 1,694,004,591 |
| | Payment of Cash Dividends | - | - |
| | Net Change in Other Borrowings | - | - |
| | Others | | - |
| | ***Net Cash Provided (used) by Financing Acities*** | **466,110,000** | **1,694,004,591** |
| IV: | **Cash and Cash Equivalents:** | | |
| | **Net Increase/ (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | **894,928,460** | **266,234,183** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the Beginning of the Quarter/Year** | **1,699,147,277** | **1,699,147,277** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the end of the Quarter/Year** | **2,594,075,737** | **1,699,147,277** |

| ***Name and Title*** | ***Signature*** | ***Date*** |
|---|---|---|
| Joseph S. Kingazi **GENERAL MANAGER** | ......................... | 30th January 2019 |
| Anna H. Teete **SENIOR ACCOUNTANT** | ......................... | 30th January 2019 |
| Denis A. Ruhangisa **INTERNAL AUDITOR** | ......................... | 30th January 2019 |

We, the under-named, non-executive members of the board of directors, attest to the correctness of the above statements. We declare that the statements have been examined by us, and to the best of our knowledge and belief have been prepared in conformance with the instructions and are true and correct.

| ***Name*** | ***Signature*** | ***Date*** |
|---|---|---|
| 1. **R.E.Hosea, CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS** | ......................... | 30th January 2019 |
| 2. **T.H.Yarumba,VICE CHAIR PERSON BOARD OF DIRECTORS** | ......................... | 30th January 2019 |

### CONDENSED STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 31/12/2018

| Current Year | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Regulatory Reserve | General Provinsion Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Balance as at the beginning of the year** | 1,512,496,093 | 0 | -3,888,172,293 | 93,021,759 | 27,594,788 | 487,455,289 | -1,767,604,364 |
| Profit for the year | - | - | (2,623,756,656) | - | - | - | -2,623,756,656 |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 5,851,305,971 | - | - | - | - | - | 5,851,305,971 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | - | (83,925,334) | - | - | (83,925,334) |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | (26,788,339) | - | (26,788,339) |
| Others | - | - | 14,416,937.00 | - | - | (33,912,961) | (19,496,024) |
| **Balance as at the end of the current period** | **7,363,802,064** | **-** | **(6,497,512,012)** | **9,096,425** | **806,449** | **453,542,328** | **1,329,735,254** |
| **Previous Year** | | | | | | | |
| **Balance as at the beginning of the year** | **1,435,346,093** | **-** | **(3,771,725,129)** | **5,045,239** | **28,060,863** | **453,542,327** | **(1,849,730,607)** |
| Profit for the year | - | - | 29,812,961 | - | - | - | 29,812,961 |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 77,150,000 | - | - | - | - | - | 77,150,000 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | - | 87,976,520 | - | - | 87,976,520 |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | (466,075) | - | (466,075) |
| Others | - | - | (146,260,126) | - | - | 33,912,962 | (112,347,164) |
| **Balance as at the end of the previous period** | **1,512,496,093** | **-** | **(3,888,172,293)** | **93,021,759** | **27,594,788** | **487,455,289** | **(1,767,604,364)** |

### MINIMUM DISCLUSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| NUMBER | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1.0 | Current Accounts | |
| | (a) Required minimum opening balance | 100,000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type): | |
| | Individuals | 8,000 |
| | Co-operatives | 6,500 |
| | Companies | 8,000 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | 1,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | 1,000 |
| | (e) ATM min statement | 200 |
| | (f) Interim statement per page | 1,500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 1,000 |
| | (h) Cheque book | 20,000 |
| | (i) Dishonoured cheque | 40,000 |
| | (j) Special clearance | N/A |
| | (k) Counter cheque | 700 |
| | (l) Stop payment | 30,000 |
| | (m) Standing order | N/A |
| | (n) Balance enquiry | N/A |
| | (o) New ATM card issuance | 10,000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | 10,000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | N/A |
| | (r) Unarranged overdraft | N/A |
| | (s) Interbank transfer | 13,000 |
| | (t) Bill payments through ATM | 1,000 |
| | (u) Deposit fee i.e for school fees | 1,000 |
| | (v) Withdrawal without cheque leaf | 5,000 |
| | (w) Withdrawal charges above 6 million | 0.15% |
| 2.0 | Savings Accounts (Disclosure for product specific types) | |
| | (a) Required minimum opening balance | 30,000 |
| | (b) Monthly service fee | 1,000 |
| | (c) Interim statement | 1,500 |
| | (d) Account closure | 10,000 |
| | (e) School fees deposite charges | 1,000 |
| | (f) ATM withdrawal fee | 1,000 |
| | (g) Withdrawal charges over the counter | 600 |
| | (h) Replacement of ID Card | 5,000 |
| | (i) Withdrawal above 3 million without notice | 0.25% |
| | (j) Stop payment charges | 30,000 |
| | (k) Salary processing fee | 3,000 |
| | (l) Pension processing fee | 2,000 |
| | (m) Searching past records fee | 10,000 |
| | (n) Dormant Account Activation | 10,000 |
| | (o) Certificate of Balance | 3,000 |
| 3.0 | Electronic Banking | |
| | (a) Internet banking monthly fee | N/A |
| | (b) Internet transfer | N/A |
| | (c) SMS banking | N/A |
| | (d) Other TT/SWIFT | 13,000 |
| | (e) Transfer from bank account to mobile | 1,000 |
| 4.0 | Foreign Exchange Transaction | N/A |
| | (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | N/A |
| | (b) Purchase of foreign cheque | N/A |
| | (c) Sale/purchases of cash passport | N/A |
| | (d) Telegraphic transfer | N/A |
| | (e) Telex/SWIFT | N/A |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | N/A |
| 5.0 | Personal Loans | |
| | (a) Processing /Arrangement/Appraisal fee | 1.5-4% |
| | (i) Personal loans | 24% |
| | (ii) Overdrafts | 18-24% |
| | (iii) Mortgage finance | N/A |
| | (iv) Asset finance | N/A |
| | (b) Unpaid loan instalment i.e. above the existing rate | 5% |
| | (c) Early repayment | N/A |
| | (d) Valuation fees | N/A |
| | (e) Discharge of Security Document to other banks | 120,000 |
| | We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information. | |

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Joseph S. Kingazi | General Manager | | 30th January 2019 |
| 2 | Anna H. Teete | Senior Accountant | | 30th January 2019 |
| 3 | Denis A. Ruhangisa | Internal Auditor | | 30th January 2019 |

215033202

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NI PERISIC AU SUAREZ RASMI ARSENAL KESHO?

**LONDON,** England

WAKATI Unai Emery akiamini Arsenal inajitahidi kadri iwezekanavyo ili kufanya usajili mpya kabla ya dirisha dogo kufungwa kesho saa sita usiku, Mtendaji Mkuu wa Inter, Giuseppe Marotta ameweka wazi kuwa klabu hiyo ya Serie A haijapokea ofa yoyote kwa Ivan Perisic.

Kumekuwapo na tetesi za Perisic kujiunga na Arsenal wakati huu pia klabu hiyo ya Kaskazini mwa London ikivutiwa kuipata huduma ya winga wa Barcelona, Denis Suarez.

Perisic alitupwa nje ya kikosi kilichoivaa Torino Jumapili kufuatia kuwasilisha ombi la kuondoka katika dirisha hili dogo.

"Ni vigumu kumbakisha mchezaji anayetaka kuondoka," Moratta aliambia Sky Sport juzi, Jumatatu.

"Lakini kwa wakati huu hakuna ofa kwa Perisic."

Winga huyo wa kimataifa wa Croatia, Perisic, 29, amekuwapo Inter tangu mwaka 2015 na hivi karibuni alihusishwa sana na Manchester United.

Lakini Emery Jumatatu aliulizwa kuhusu majina yote mawili; Perisic na Suarez, kuelekea mechi yao ya nyumbani jana kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Cardiff City na ingawa kocha huyo wa Arsenal hakuwa tayari kutaja mchezaji mmojawapo, yupo tayari kuona sura mpya ikitua wiki hii.

"Ni kitu ambacho klabu inakifanyia kazi, uwezekano wa wachezaji tofauti," aliuambia mkutano wa wanahabari.

"Sijui moja kwa moja ni wachezaji gani, lakini wachezaji watakaoweza kutusaidia, ambaye anaweza kucheza winga, kulia ama kushoto. Nadhani mchezaji yeyote anayeweza kuja hapa na kutusaidia sisi ni habari njema.

"[Suarez] ni sawa na [kama Perisic]. Uhamisho huu si rahisi na ujumbe ni kwamba klabu inafanyia kazi wachezaji tofauti. Uwezekano kama inawezekana [kukamilika], ni vizuri kwetu.

"Sijui [nini kitatokea] kwa sababu dirisha hili la usajili si rahisi. Ninajua klabu inafanya vyovyote iwezavyo kupata mchezaji mmoja wa kutusaidia."

Emery alithibitisha, kwa ujumla Arsenal inatazama wachezaji wawili na kuweka matumaini wote wanaweza kutua, akiongeza: "Kati ya hakuna na [kusajili] wawili. Wawili kwa sababu tunatazama wachezaji wawili tofauti ambao wanauwezekano wa kuja hapa."

Arsenal inakabiliwa na tatizo la majeruhi katika safu ya ulinzi, kufuatia Laurent Koscielny na Sokratis Papastathopoulos kukosekana jana, lakini bado Emery haamini usajili mwingine unahitajika katika idara ya ulinzi.

"Tunaweza kuleta wachezaji ambao tunashawishika watakuwa tayari kutusaidia wenye kiwango kizuri," alisema. "Tunao wachezaji wakutosha ambao wanaweza kucheza nafasi ya beki wa kati kikosini.

## KWA UFUPI

### CAHILL ANUKIA ARSENAL
ARSENAL inataka kumsajili beki wa kati wa zamani wa England, Gary Cahill, 33, ili kusaidia matatizo ya majeruhi katika safu ya ulinzi. **(Mirror)**

### GUEYE AOMBA KUONDOKA
KIUNGO wa Everton, Idrissa Gueye, 29, ambaye klabu yake hiyo imeikataa ofa ya pauni milioni 21.5 kutoka Paris St-Germain, anataka kuondoka Goodison Park club. **(Mail)**

### RAKITIC AWINDWA CHELSEA
CHELSEA inataka kumsajili kiungo wa Croatia na Barcelona, Ivan Rakitic, 30, katika majira ya joto. **(Sport, via Express)**

### MAN CITY KUTUA LEICESTER
MANCHESTER CITY inavutiwa kumsajili beki wa Leicester na England, Ben Chilwell, 22, katika majira haya ya joto. **(ESPN)**

### MANE AFUNGUKA MADRID
WINGA wa Liverpool na Senegal, Sadio Mane, 26, amesema 'Wekundu' hao wa Anfield ndio wenye "wasiwasi tu" wakati huu kukiwa na tetesi za yeye kutua Real Madrid. **(World Soccer)**

### BENITEZ HAONDOKI NEWCASTLE
RAFAEL Benitez, ambaye mkataba wake na Newcastle unamalizika mwishoni mwa msimu, amesema itakuwa "vigumu sana" kwake yeye kuondoka Magpies baada ya dirisha la usajili la Januari kufungwa kesho. **(Sun)**

### UNITED YAIACHIA ARSENAL
MANCHESTER UNITED walivutiwa na winga wa Inter Milan, Ivan Perisic chini ya kocha wa zamani Jose Mourinho, lakini haijiandai kuingia katika mbio za kumwania Mcroatia huyo na Arsenal baada ya Mreno huyo kuondoka Old Trafford. **(Evening Standard)**

### MATA AFUNGWA UNITED
MANCHESTER UNITED imempa ofa ya mkataba wa mwaka mmoja kiungo Mhispania Juan Mata, 30, ili kumzuia kuondoka bure. **(Mirror)**

### SPURS, PSG VITANI
TOTTENHAM inapanga kutoa ofa ya pauni milioni 30 majira ya joto kwa kiungo wa Valencia, Carlos Soler, 22, ambaye pia anawindwa na PSG. **(ESPN)**

### CITY KUMUUZA MATONDO
MANCHESTER CITY imekubali kumuuza winga raia wa Wales, Rabbi Matondo, 18, kwa pauni milioni 11.29 kutoka Schalke ya Ujerumani. **(Telegraph)**

### WENGER KAITOBOA ARSENAL
KOCHA aliyeondoka Arsenal, Arsene Wenger pamoja na benchi lake la ufundi, wameigharimu 'Gunners' pauni milioni 17.1. **(Times)**

### LEICESTER YAMGOMEA FUCHS
LEICESTER imeikataa ofa kutoka kwa Aston Villa ya kumsajili kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu beki wa kushoto, Christian Fuchs, 32. **(Sky Sports)**

# HABARI MICHEZO

## SportPesa Cup yaacha neema

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mchezaji wa zamani wa Everton ya England na timu ya Taifa ya Afrika Kusini, Steven Pienaar, akieleza kukunwa na viwango vilivyoonyeshwa kwenye michuano ya SportPesa Cup iliyomalizika mwishoni mwa wiki kwa timu ya Kariobangi Sharks kutwaa ubingwa, kinyang'anyiro hicho kimeleta neema Tanzania, Kenya na Afrika Kusini.

Pienaar ambaye ni balozi wa Everton wakati wa ziara yake hiyo, alishiriki kwenye kugawa vifaa vya michezo kupitia Kampeni ya 'Kits for Africa' yenye lengo la kuwanufaisha zaidi ya wachezaji chipukizi 200.

Kwa msimu huu, SportPesa imeweza kukusanya vifaa zaidi ya 45,000 ambavyo vitagawiwa nchi za Kenya, Tanzania na Afrika Kusini.

Akizungumzia michuano hiyo, Pienaar alisema: "Ilikuwa ni furaha kuona ni kwa jinsi gani ushirikiano baina ya SportPesa na Everton umekuwa na umuhimu kwa jamii ambayo inaishi kwenye mazingira magumu hapa Tanzania. Kits for Africa ni moja tu ya kampeni ambayo SportPesa imekuwa ikiendesha ili kukuza fursa ya vipaji vya baadaye hapa Afrika Mashariki."

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alisema: "michuano hii ni muhimu na maalum kwa wanafamilia wa mpira wa miguu kwani inatoa fursa kuonyesha vipaji vyao.

"Vile vile kwa timu bora kutoka Kenya na Tanzania kucheza pamoja, ilikuwa ni muda wa kuonyesha vipaji vya mpira barani Afrika na kukuza mchezo huo kwenye ukanda huu."

## ZFA kuchaguana Februari mwishoni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Soka Zanzibar (ZFA), kinatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu mwishoni mwa Februari mwaka huu kwa kutumia katiba mpya ambayo tayari imeshasambazwa kwa wadau wa soka visiwani hapa wakati huo ikisubiriwa kupitishwa katika mkutano mkuu.

Mkutano huo mkuu utafuatiwa na uchaguzi huo wa viongozi wa chama hicho chenye majukumu ya kusimamia na kuendesha mchezo wa soka Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Kamati ya Maridhiano ya Chama hicho, Mohammed Ali Hilali 'Teddy', alisema uchaguzi huo utaanzia katika ngazi za wilaya na kumalizikia ngazi ya Taifa kwa nafasi ya Urais pamoja na Makamu wa Rais.

Aidha, alisema bado tarehe rasmi ya uchaguzi huo haijapangwa, lakini hadi mwisho mwa mwezi ujao lazima uchaguzi huo ufanyike na viongozi watakaochaguliwa waanze kuongoza kwa mujibu wa katiba hiyo mpya ambayo itapitishwa katika mkutano mkuu.

"Bado hatujapanga tarehe rasmi ya uchaguzi, lakini utafanyika 'Inshallah' maana muda wa kamati wa maridhiano umeagizwa hadi Februari uchaguzi uwe umeshafanyika,"alisema .

# TFF YAFUNGUKA UCHAGUZI YANGA

**Na Faustine Feliciane**

UCHAGUZI wa klabu ya Yanga ambao umekuwa ukirushwa kila mara, sasa utafanyika baada ya kufanyika kwa uchaguzi mdogo wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imeelezwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Ally Mchungahela, akizungumza jana, alisema wanaamini vikwazo vyote ambavyo vilikuwapo vinaelekea kumalizika na uchaguzi huo utatajwa tena baada ya kufanyika kwa uchaguzi huo mdogo wa TFF.

TFF inatarajia kufanya uchaguzi huo mdogo wa kuziba nafasi moja ya mjumbe wa Kamati ya Utendaji Jumamosi ijayo jijini Arusha.

"Niseme tu uchaguzi wa Yanga utafanyika, maelezo ya lini utafanyika tutasema baada ya uchaguzi mdogo wa TFF, nitafanya kikao na waandishi wa habari baada ya hapo ili kutoa maelezo," alisema Mchungahela.

Aidha, alisema uchaguzi huo utafanyika kwa kushirikiana na Kamati ya Utendaji ya Yanga ambayo itatoa watu wa kuungana na Kamati ya Uchaguzi ya TFF kusimamia na kufanikisha uchaguzi huo.

Awali Yanga walikuwa wafanye uchaguzi wao Januari 13, mwaka huu, lakini uchaguzi huo ulisimamishwa na mahakama baada ya baadhi ya wanachama wa klabu hiyo kufungua kesi mahakamani kupinga mchakato wa uchaguzi huo.

Wanachama hao walipinga TFF kuusimamia uchaguzi huo wakati klabu hiyo ina katiba yake inayoeleza mchakato wa uchaguzi wa viongozi wake unavyokuwa.

**16-BORA...**




Wchezaji wa Azam, ambao juzi timu yao ilifanikiwa kutinga hatua ya 16-Bora ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania maarufu FA Cup kwa kuichapa Pamba ya Mwanza kwa mabao 2-0 katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam. **PICHA: BIN ZUBEIRY**

# Okwi: Tutaivaa Al Ahly kwa tahadhari Misri

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Emmanuel Okwi (pichani), amesema wanafahamu ugumu uliopo katika mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Msiri, hivyo watacheza kwa tahadhari kubwa kwenye mechi hiyo ya ugenini.

Okwi, aliliambia Nipashe jana kabla ya timu hiyo kukwea pipa kuelekea Misri, kwamba wanawafahamu Al Ahly ni timu kubwa na bora, lakini hawatakuwa wanyonge mbele yao.

Alisema wapo mashabiki ambao tayari wana matokeo yao mkononi hasa baada ya kufungwa mchezo uliopita mabao 5-0 dhidi ya AS Vita ya Congo, lakini kwenye soka lolote linaweza kutokea ndani ya dakika 90.

"Tunatakiwa kuwa makini muda wote wa mchezo, kocha ametupa maelekezo na tunaendelea kuyafanyia kazi kuhakikisha tunafanya vizuri," alisema nyota huyo wa kimataifa wa Uganda.

Kikosi cha Simba kilitarajia kuondoka jana usiku kuelekea Misri tayari kwa mchezo huo wa Kundi D utakaochezwa Jumamosi ijayo.

Simba kwenye kundi hilo tayari imecheza michezo miwili na kufanikiwa kushinda mechi moja dhidi ya JS Saoura ya Algeria kabla ya kupoteza ugenini dhidi ya AS Vita.

Matokeo hayo yameifanya Simba kushika nafasi ya tatu ikiwa na pointi tatu sawa na AS Vita inayoshika nafasi ya pili, lakini ikiwa na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa, Al Ahly inaongoza kundi ikiwa na pointi nne huku JS Saoura wakiburuza mkia kwa pointi moja.



# Michezo

Jumatano Januari 30, 2019

Nipashe


## Ni Perisic au Suarez rasmi Arsenal kesho?



HABARI UK. 30

OKOA...



Mabeki wa kati wa Real Madrid, Sergio Ramos na Raphael Varane, wakiruka kuwahi kuokoa mpira kwa kichwa dhidi ya washambuliaji wa Espanyol kwenye mechi ya La Liga iliyopigwa usiku wa kuamkia juzi katika Uwanja wa RCDE. Real Madrid ilishinda 4-2. **PICHA: MTANDAO**

# ZAHERA AITISHA SIMBA

## Awatumia Boban, Banka kuipa jeuri Yanga wakati huu wakijiandaa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikikwea pipa jana kuelekea Alexandria, Misri kwa ajili ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly, Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera amesema tayari amepata dawa ya kuwadhibiti mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara.

Simba ambayo imeondoka jana usiku kuelekea Misri katika mechi hiyo ya hatua ya makundi, itashuka dimbani Jumamosi saa 4:00 kwa saa za Afrika ya Mashariki kucheza mechi yao ya tatu katika Kundi D.

Hata hivyo, kama hapatatokea mabadiliko, kwa mujibu wa ratiba ya Ligi Kuu Bara, Simba na Yanga zitakutana Februari 16, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika kipindi cha michezo cha Redio One juzi, Zahera alisema ana uhakika wa kufanya vizuri watakapokutana na Simba mwezi ujao kutokana na namna alivyokiimarisha kikosi chake.

Alisema uwapo wa wachezaji wawili, Mohamed Issa Banka na Haruna Moshi 'Boban' waliongeza nguvu katika kikosi chake, anaimani watasaidia kuisimamisha Simba watapaokutana Februari 16.

"Mechi haiwezi kuwa kama ilivyokuwa mzunguko wa kwanza, nina uhakika Boban na Banka watatusaidia sana tutakapokutana.

"Ukiangalia tu wanavyofanya mazoezi na namna walivyoongeza nguvu kikosini, ninaamini tunaweza kushinda mechi hiyo," alisema Zahera.

Boban ametua Yanga katika usajili wa dirisha dogo akitokea African Lyon wakati Banka aliyesajiliwa katika dirisha kubwa akitokea Mtibwa Sugar alikuwa nje ya uwanja kwa kipindi cha miezi 14 akitumikia adhabu ya kutumia dawa zisizoruhusiwa michezoni.

Kamati ya Kuzuia na Kupambana na Dawa zisizoruhusiwa michezoni ya Kanda ya Tano Afrika (RADO), ilitoa hukumu ya kumfungia Banka kutokana na kutumia Bangi.

Kutokana na kosa hilo, Banka alitakiwa kutoa maelezo ikiwamo kukataa au kukubali kosa ambapo alikubali na baada ya uchunguzi wa maabara na utetezi kutoka kwa mchezaji huyo, kamati ilimkuta na hatia hivyo kumfungia kwa kipindi cha miezi 14 kuanzia Desemba 9, 2017 na adhabu hiyo inatarajiwa kumalizika Februari 8, mwaka huu, na kuanzia hapo atakuwa huru kuanza kuitumikia Yanga.

Kwa kipindi chote cha adhabu hiyo, Banka hakuruhusiwa kufanya chochote kinachohusiana na mpira wa miguu, ikiwamo kufanya mazoezi hadharani au kuonekana akishiriki shughuli za soka.

## Simba SC wapewa mbinu za Waarabu

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kikosi cha Simba kikiondoka jana usiku kuelekea Misri tayari kwa mchezo wao wa Kundi D wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly, wachezaji wa timu hiyo wamepewa mbinu ya kuwakabili Waarabu hao ugenini.

Inafahamika Waarabu wamekuwa na mbinu nyingi ndani na nje ya uwanja pindi wanapocheza nyumbani dhidi ya timu nyingine.

Beki na naodha wa zamani wa Simba, Boniface Pawasa, ameiambia Simba kuwa ili iweze kufanya vema kwenye mchezo huo, wanapaswa kuzikabili mbinu za Waarabu hao.

**Alisema tangu wakati akiwa mchezaji wa Simba anafahamu namna Waarabu wanavyocheza wanapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani.**

"Wachezaji wa Simba na makocha wao lazima wafahamu Waarabu wakiwa nyumbani watashambulia sana dakika 20 za kwanza wakijaribu kusaka bao la mapema, Simba wanatakiwa kuwa makini katika dakika hizo," alisema Pawasa.

"Lakini pia Waarabu wana kawaida ya kupoteza muda pindi wanapokuwa mbele kwa mabao..., na tabia nyingine ni kupenda 'kuchokoza' wachezaji wa timu pinzani ili kuwatia hasira wafanye vitendo ambavyo vitawasababishia kupata adhabu kutoka kwa mwamuzi, wachezaji wa Simba lazima wawe makini na vitendo hivi, wanapaswa kuhakikisha hawawapi nafasi na wala wasijibishane na mwamuzi pindi anapopiga filimbi ya faulo," alisema Pawasa.

Aidha, nyota huyo wa zamani wa timu ya Taifa 'Taifa Stars', alisema kama kocha na wachezaji wa Simba watakuwa na nidhamu ya mchezo muda wote na kuepuka hila za wapinzani wao wanaweza wakafanya vizuri.

Simba itashuka uwanjani kukabiliana na wapinzani wao hao Jumamosi ukiwa mchezo wao wa tatu katika kundi lao.

Kocha wa Simba, Patrick Aussems, akizungumza na gazeti hili juzi, alisema anafahamu ugumu wa mchezo huo hasa kutokana na kucheza ugenini na tayari amewapa maelekezo wachezaji wake.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >